**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**TUME YA MIPANGO ZANZIBAR**

# MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026

## KITABU CHA PILI

**JUNI, 2025**

## YALIYOMO:

**Mada** **Ukurasa**

**1.0 UTANGULIZI ..........1**
**2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025 ..........2**
2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia. ..........2
2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ..........3
2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. ..........4
2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki ..........4
2.5 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei wa Dunia ..........5
**3.1 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2025 ..........6**
**5.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWAMWAKA 2025/2026 ..........8**
**6.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2025/2026 ..........8**
**7.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026..........10**
**8.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO KWA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2025/2026 ..........12**
8.1 Ofisi ya Rais Ikulu ..........12
8.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji ..........14
8.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango ..........16
8.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar ..........18
8.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ..........21
8.3.3 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ..........22
8.4 Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ..........23
8.4.1Mahkama Kuu ..........25
8.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ..........27
8.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ..........31
8.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) ..........32
8.5.2 Kikosi cha Valantia ..........32
8.5.3 Chuo cha Mafunzo ..........33
8.5.4 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ..........34
8.5.5 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ..........35

8.6 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ....................................................36
8.6.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA)....................................37
8.6.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ...........38
8.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi....................................................................................................39
8.8 Wizara ya Afya.......................................................................................40
8.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ..........................................47
8.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda......................................48
8.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali..................................................49
8.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.................................52
8.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ............................53
8.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ......................61
8.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini........................................................62
8.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi .................................................68
8.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.........................................72
8.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale......................................................78
**9.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI..........................................................79**
**10.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO.....................................................80**
**11.0 HITIMISHO .......................................................................................80**

**Orodha ya Viambatisho**

Kiambatisho 1: Mgao wa Fedha za Programu na Miradi ya Maendeleo 2025/26 Kiwizara.

# 1.0 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026 umeandaliwa kwa mujibu wa Ibara ya 10 (3) (c) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Sheria ya Tume ya Mipango ya 2012 kifungu namba 11. Mpango huu umeandaliwa kwa lengo la kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050, ambayo ni kuiwezesha Zanzibar kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati (Middle Income Status).

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (ZADEP), 2021-2026 tunakamilisha utekelezaji wake katika mwaka 2025/2026. Mpango huu umetekelezwa kwa kuzingatia shughuli za Uchumi Buluu kwa Ukuaji wa Maendeleo Jumuishi na Endelevu.

Ili kuyafikia maendeleo ya kweli ushirikiano wa wadau mbali mbali ni njia muhimu ya Serikali na Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na wananchi wana wajibu wa kujenga uchumi na kulinda rasilimali zilizopo kwa kuunga mkono juhudi za Serikali. Mipango ya maendeleo iliyowazi na Sera madhubuti zinaleta maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Tume ya Mipango inafanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026 ambao unatarajiwa kufika ukomo mwaka 2025/2026. Mapitio ya ZADEP yataonesha njia na mwelekeo wa Mpango wetu wa Awamu ya Pili ambao utekelezaji wake utaanza Julai 2026. Matayarisho ya kuwa na Mpango Mpya wa Maendeleo wa Awamu ya Pili yameanza ili kuendelea na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050.

Katika kipindi cha mwaka 2025, uchumi unatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.3 na mfumko wa bei unatarajiwa kubakia katika tarakimu moja chini ya kiwango cha asilimia 5. Vichocheo vya ukuaji huo ni pamoja na: Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha; Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo; Kuimarisha mazingira rafiki kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ili kupunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu; Kuimarisha uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ili kuongeza usarifu wa bidhaa mbali mbali kwa ajili ya kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi; Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;

Kuanza kwa utekelezaji wa miradi wezeshi kwa Zanzibar kuwa mwenyeji wa baadhi ya mechi za Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Africa (AFCON) 2027; na Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/2026 utaendelea kuimarisha maeneo ya kukuza uchumi na ustawi wa kijamii kwa ujenzi wa miundombinu ya usafiri, kilimo, kuongeza ajira hususan kwa vijana, kuimarisha ubora wa elimu, kuimarisha huduma za afya, upatikanaji wa maji safi na salama na kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, magonjwa ya mripuko na mafuriko. Mkazo zaidi utawekwa katika kuimarisha miundombinu ya utalii ikiwemo maeneo ya kihistoria; Ujenzi wa bandari ya uvuvi Shumba, bandari jumuishi – Mangapwani na bandari ya abiria na mizigo Maruhubi; Viwanda vya kuchakata na kusarifu samaki; Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya msingi ya barabara, viwanja vya ndege, maji na nishati; Kuendeleza maeneo maalum ya viwanda, vituo vya biashara na maonesho, mageuzi ya sekta ya kilimo na mageuzi ya kidigitali; Kuimarisha miundombinu na ubora wa elimu, afya, viwanja vya michezo pamoja na maendeleo ya makaazi; na Kuimarisha utawala bora na uhimilivu kwa kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Zanzibar salama, ujenzi wa Mahkama za Wilaya na Mikoa, uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Kitabu hiki kinaelezea Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026 kwa kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021-2026, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika ufunguzi wa Baraza la kumi (10) la Wawakilishi. Pia mpango huu umezingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) ya Mwaka 2030; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; pamoja na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063 (African Development Agenda) .

## 2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2025

### 2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Januari 2025 na Shirika la Fedha la Kimataifa

(IMF), uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kuimarika na kufikia kiwango cha wastani wa ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2025, ukilinganisha na asilimia 3.2 mwaka 2024. Ukuaji huu utatokana na kuongezeka kwa kasi ya uchumi wa nchi zilizoendelea hasa kwa nchi ya Marekani, ambayo inatarajiwa uchumi wake kukua kwa asilimia 2.7. Aidha, Mataifa mengine makubwa kama vile China, Japan na nchi za Umoja wa Ulaya pia yanatarajiwa kuimarika zaidi katika shughuli za kibiashara.

**Kwa Nchi Zilizoendelea,** kasi ya ukuaji inatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.7 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za Umoja wa Ulaya unatarajiwa kuimarika kufikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2025 kutoka ukuaji wa asilimia 1.0 mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa matumizi na uwekezaji baada ya mdororo wa uchumi mwaka 2024, uliotokana na ongezeko la viwango vya riba vilivyotekelezwa na Benki Kuu za nchi hizo katika jitihada za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei pamoja na machafuko ya kisiasa kati ya Urusi na nchi za Magharibi, zilichochea kupanda kwa gharama za uzalishaji na kupunguza kasi ya ukuaji wa viwanda barani Ulaya.

**Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi** (Emerging Market and Developing Economies), unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025 ukilinganisha na ukuaji kama huo mwaka 2024. China ni moja ya Nchi ambayo inaongoza katika kuchangia ukuaji wa Uchumi wa Nchi hizi, kwa mwaka 2025 Uchumi wa China, unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.5 mwaka 2025. Ukuaji huu utatokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali ya China katika kuimarisha mahitaji ya ndani na kushajihisha sekta binafsi kuongeza uzalishaji. Hata hivyo, vita vya kibiashara za kimataifa baina ya Marekani na Nchi za Brazil, Russia, India, China na South Africa (BRICS) vinaweza kupunguza matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi. Mkakati wa Marekani wa kuongeza ushuru kwa Nchi nyingi zinazoibukia kiuchumi zikiongozwa na China (asilimia 145), kunaweza kuathiri ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo.

## 2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika

Uchumi wa Bara la Afrika unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.1 kwa

mwaka 2025, ukilinganishwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2024, kasi hii ya ukuaji, inatatokana na uwekezaji katika sekta ya nishati, pamoja na ongezeko la usafirishaji wa mafuta na gesi kutoka nchi wazalishaji wa mafuta wakubwa barani Afrika kama Zimbabwe, Nigeria, Libya, Angola na Algeria ambayo inatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2025. Senegal na Ivory Coast zinatarajiwa kuwa na ukuaji wa zaidi ya asilimia 6.0 kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu, sekta ya kilimo na kuongezeka kwa matumizi ya ndani. Aidha, maendeleo ya kiteknolojia na utekelezaji wa miradi ya nishati mbadala katika baadhi ya nchi za Afrika Mashariki na Afrika Magharibi, kama Kenya na Ghana, yanatarajiwa kuongeza ukuaji wa Uchumi wa nchi za Bara la Afrika.

Hata hivyo, matarajio hayo ya ukuaji wa uchumi barani Afrika yanaweza kuathirika kutokana na mabadiliko ya sera za biashara za kimataifa kutoka Marekani, ikiwemo kubadilika kwa Mikataba ya biashara za kimataifa juu ya usafirishaji bidhaa kutoka Nchi za Afrika kwenda katika soko la Marekani, zikiwemo Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuchumi Kusini mwa Africa (SADC).

### 2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub-Saharan Afrika) unatarajiwa kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2024. Ukuaji huu utatokana na kuimarika kwa uzalishaji wa nishati mbadala, kuongezeka kwa uwekezaji wa ndani na wa nje. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi katika baadhi ya nchi kama vile Ethiopia, Ivory Coast na Senegal, inatarajiwa kukua kwa zaidi ya asilimia 5.0 mwaka 2025, kutokana na uwekezaji katika miundombinu, usafirishaji, kilimo, kuimarika kwa huduma za kidijitali pamoja na kuwepo kwa mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

### 2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2025 unatarajiwa kuimarika na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Ongezeko hilo litatokana na mikakati ya

mageuzi ya kiuchumi yaliyozinduliwa ambayo yanalenga kutatua changamoto za kiuchumi, kuimarisha sekta za uzalishaji na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi. Vile vile, kuongezeka kwa matumizi ya dijitali yanayopelekea kuongezeka kwa masoko mapya ya biashara na wawekezaji.

Kwa kuangalia mwenendo wa uchumi kwa Nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2025, Uchumi wa **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, unatarajiwa kukuwa kufikia wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuimarika kwa miundombinu na kuwepo kwa Sera za kukuza maendeleo endelevu. Uchumi wa **Uganda** unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.5 kwa mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuanza uzalishaji wa mafuta na kuwepo kwa uwekezaji katika sekta mbalimbali. Nchi ya **Burundi** uchumi unatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 3.5 kwa mwaka 2025 kutoka asilimia 4.6 mwaka 2024. Upungufu huu utatokana na kupungua kwa mahitaji ya ndani, uzalishaji pamoja na kupungua kwa mapato ya mauzo ya nje kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa. Kwa upande wa Nchi ya **Rwanda** ukuaji wa Uchumi unatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2024. Hii ni kutokana mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri kilimo, kutokuwa na mashirikiano mazuri na nchi wanachama wa kibiashara. Hata hivyo, uchumi wa Nchi ya **Kenya** unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2025 kutoka asilimia 5.2 mwaka 2024. Hii itatokana na kuimarika kwa sekta ya huduma, kuongezeka kwa mauzo ya nje ya bidhaa za kilimo na kuimarika kwa fedha za nje.

### 2.5 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumko wa bei Duniani inatarajiwa kupungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2024. Kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei Duniani kutatokana na kurejea kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma katika Nchi za Umoja wa Ulaya na China. Hata hivyo, kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kuongezeka kwa nchi ya Marekani ikiwa wataendelea kutekeleza Sera ya kuongeza ushuru wa bidhaa zinazoingizwa kutoka Nchi washirika wa biashara duniani.

Kwa upande wa Nchi Zilizoendelea kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 2.0 kwa mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 na kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi mfumko wa bei unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2024.

## 3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2025

Uchumi wa Zanzibar mwaka 2025 unatarajiwa kuimarika zaidi, sekta zinazotarajiwa kukua kwa kasi kubwa zaidi ni pamoja na sekta ya miundombinu, biashara, uwekezaji, sekta za huduma na viwanda.

**Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2025**

Shabaha za Uchumi Jumuishi zilizozingatiwa kwa mwaka 2025 ni kama ifuatavyo:-

i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.3 kutoka ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2024;
ii. Mfumko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa Nchi za Afrika Mashariki;
iii. Uwiano wa Mapato ya ndani kufikia asilimia 33.4 ya Pato la Taifa mwaka 2025 kutoka asilimia 26 mwaka 2024;
iv. Uwiano wa Mapato ya kodi kufikia asilimia 33 ya Pato la Taifa mwaka 2025 kutoka asilimia 22.4 mwaka 2024;
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0;
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi mitatu;
vii. Pato la mwananchi kuendelea kubakia juu ya wastani wa Dola za Kimarekani 1,449.

Matarajio ya Shabaha za ukuaji wa uchumi utatokana na sababu zifuatazo:-

i. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 12.6 kutoka watalii 736,755 kwa mwaka 2024 hadi watalii 829,929 mwaka 2025;
ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Unguja na Pemba, ujenzi wa bandari ya Mangapwani na ukarabati

wa bandari ya Malindi. Miradi mengine ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii. Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumko wa bei ili kubakia katika tarakimu moja;
iv. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato kidigitali na usimamizi wa matumizi ya Serikali;
v. Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje;
vi. Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kuwawekea mazingira mazuri ya uwekezaji na upatikanaji wa huduma ;
vii. Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu na kuimarisha matumizi endelevu ya Bahari ikiwemo uchakataji wa mazao ya baharini baada ya kukamilika ujenzi wa viwanda; na
viii. Kuongezeka kwa miradi ya maendeleo baada ya kupatikana kwa fedha zilizotokana na uwekezaji wa mitaji kwa njia ya Sukuk.

Ukuaji wa uchumi utatokana na misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;
iv. Kuimarisha uwekezaji katika sekta ya viwanda na kuongeza thamani kwa usafirishaji wa bidhaa zilizochakatwa nje ya nchi;
v. Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha baadhi ya mechi za Mashindani ya Kombe la Africa (AFCON) 2027;
vi. Kutumia fursa za kiuchumi za mashindano ya wachezaji wa ndani wa Afrika (CHAN) zinazotarajiwa kuanza mwezi Agosti 2025; na
vii. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo:-

i. Kuendelea kuweka bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula, nishati (Petroli, Dizeli na Mafuta ya taa) na vifaa vya ujenzi;
ii. Kuendelea kuimarisha mazingira kwa kukaribisha sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;
iii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei;
iv. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani;
v. Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;
vi. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na
vii. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku kwa bidhaa muhimu za vyakula.

## 4.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026

Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 umetayarishwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 na Hotuba ya ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi. Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026 pia umezingatia Maelekezo ya Serikali kiujumla, ahadi zinazotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi pamoja na maagizo ya viongozi wakuu wa Nchi. Mpango huu umezingatia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo yenye kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali ili kuleta matokeo ya haraka katika kufikia maendeleo ya Zanzibar na ustawi wa wananchi.

## 5.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2025/2026

Kwa mwaka 2025/2026, Serikali inaendelea na mkakati wa kuleta mapinduzi ya kiuchumi na kijamii Zanzibar kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika maeneo ya uzalishaji, kugharamia utoaji wa huduma muhimu za kijamii

ikiwemo afya, elimu, maji, umeme, kuimarisha utalii na uwekezaji kwa lengo la kuinua kipato cha mwananchi, kuongeza ajira na kukuza uchumi wa Zanzibar kwa ujumla wake. **Miradi ya kimkakati imepangwa kwa kuzingatia faida zitakazopatikana na yenye kuleta matokeo ya haraka katika kuimarisha shughuli za kiuchumi na kuinua hali za wananchi. Kama ulivyo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021– 2026, Miradi ya kimkakati imegawanywa katika maeneo matano (5) ambayo ni: (1) Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; (2) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; (3) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (4) Kukuza Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na (5) Kuimarisha Utawala na Uhimilivu.**

i. **Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu:** Programu na Miradi inayotarajiwa kutelekezwa kupitia eneo hili ni:-
   a) Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria;
   b) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Utalii;
   c) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba;
   d) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani;
   e) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; na
   f) Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kuchakata na Kusarifu Samaki.

ii. **Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu**: Programu na Miradi inayotarajiwa kutelekezwa kupitia eneo hili ni:-
   a) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu;
   b) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani;
   c) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini;
   d) Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege;
   e) Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar;
   f) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar; na
   g) Ujenzi wa Misingi ya Maji pamoja na Matengenezo ya Maziwa katika Maeneo ya Mji.

iii. **Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi:** Programu na Miradi inayotarajiwa kutelekezwa kupitia eneo hili ni:-
   a) Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar;
   b) Programu ya Mageuzi ya Kidigitali;

c) Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Parks);
d) Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula; na
e) Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania.

**iv. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii: Programu na Miradi inayotarajiwa kutelekezwa kupitia eneo hili ni:-**

a) Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu;
b) Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Michezo;
c) Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi;
d) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja; na
e) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni.

v. **Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu:** Miradi inayotarajiwa kutelekezwa kupitia eneo hili ni:-

a) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama;
b) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Wilaya na Mikoa; na
c) Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

## 6.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026

Kwa mwaka 2025/2026, Serikali imepanga kutumia kiasi cha TZS 4,539.64 bilioni kwa kutekeleza shughuli za maendeleo kupitia programu 41 na miradi 56 ya maendeleo (Programu 7 na miradi 17 ni mipya) zitakazosimamiwa kupitia Wizara na Taasisi za Serikali Kuu. Kati ya fedha hizo, Serikali imepanga kutoa TZS 3,231.40 bilioni sawa na asilimia 71.18 ya bajeti yote ya maendeleo, ambapo TZS 2,411.00 bilioni zitatumika kugharamia programu na miradi ya kimkakati na TZS 820.40 bilioni kwa miradi mengineyo. Kiasi cha TZS 1,308.24 bilioni (TZS 962.74 bilioni ni mikopo na TZS 345.50 bilioni ni ruzuku) sawa na asilimia 28.82 ya bajeti ya maendeleo zinatarajiwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Muhtasari wa fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa Programu/Miradi ya Maendeleo kwa Maeneo Makuu Matano ya Kimkakati unaonekana katika **Jadweli nambari 1**.

**Jadweli nam.1: Muhtasari wa Mgao wa Fedha Zilizopangwa kwa Upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa Programu/Miradi Kwa Maeneo Makuu kwa Mwaka 2025/2026**

| ENEO | MAKISIO KWA MWAKA 2025/2026 (TZS "000") | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **SMZ** | **%** | **RUZUKU** | **MKOPO** | **JUMLA YA FEDHA ZA WASHIRIKA WA MAENDELEO** | **%** | **JUMLA YA BAJETI YOTE** | **%** |
| **ENEO 1:** Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu | 348,345,734 | 69 | 132,698,000 | 23,138,491 | 155,836,491 | 31 | 504,182,225 | 11 |
| **ENEO 2:** Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu | 728,190,201 | 60 | 76,297,823 | 419,181,945 | 495,479,768 | 40 | 1,223,669,969 | 27 |
| **ENEO 3:** Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi | 164,538,645 | 81 | 9,926,385 | 27,956,218 | 37,882,603 | 19 | 202,421,248 | 4 |
| **ENEO 4:** Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii | 1,188,666,100 | 69 | 95,083,448 | 430,556,669 | 525,640,117 | 31 | 1,714,306,217 | 38 |
| **ENEO 5:** Utawala Bora na Uhimilivu | 801,659,320 | 90 | 31,492,372 | 61,908,827 | 93,401,299 | 10 | 895,060,619 | 20 |
| **JUMLA KUU** | **3,231,400,000** | **71** | **345,498,027** | **962,742,151** | **1,308,240,178** | **29** | **4,539,640,178** | **100** |

## 7.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO KWA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2025/2026

### 7.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Rais Ikulu ni Taasisi inayosimamia shughuli za Kiongozi Mkuu wa Taifa na utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Zanzibar. Ofisi pia inaratibu shughuli zinazotekelezwa na Baraza la Mapinduzi ikiwa ni chombo cha juu Serikalini cha kufanya maamuzi na kutoa maelekezo na miongozo. Ofisi ya Rais pia inaratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi (Diaspora). Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais Ikulu imepanga kutekeleza Miradi mitatu ya Maendeleo kwa gharama ya TZS 8.70 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Ikulu***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha majengo ya Ikulu ili kuwa na makazi mazuri yenye hadhi za Viongozi Wakuu. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza na ujenzi wa Ofisi na nyumba katika eneo la Ofisi za Ikulu – Bwefum.

***Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweka mifumo iliyoimara ya ulinzi na usalama. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha Mifumo ya Ofisi;
ii. Kuimarisha kitengo cha Teknolojia ya Habari kwa ununuzi na ufungaji wa vifaa vya Teknolojia ya Habari; na
iii. Uimarishaji wa Mfumo wa Kamera za kisasa (Closed Circuit Television CCTV).

*Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano ya Mfumo wa Sema na Rais (SNR)*

Mradi una lengo la kuhakikisha kuwa na njia rahisi, za kisasa na zenye ufanisi kwa wananchi kufikisha maoni, malalamiko, mapendekezo na maswali yao moja kwa moja kwa Rais au Ofisi ya Rais, kwa lengo la kukuza uwazi na uwajibikaji wa Serikali. Vile vile, kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati na kukuza ushirikishwaji wa wananchi katika masuala ya uongozi na maendeleo ya Taifa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 700.00 milioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ununuzi wa teknolojia za kisasa za mawasiliano;
ii. Kujenga uelewa kwa wananchi kuhusiana na matumizi sahihi ya mfumo wa SNR; na
iii. Kufanya tathmini ya matumizi ya mfumo wa SNR kwa kipindi cha miaka minne tokea kuanzishwa kwake kutoka mwaka 2021 hadi 2025.

### 7.1.1 Taasisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Serikali

Taasisi hii ni chombo kilichoanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kusaidia, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia muda wa utekelezaji na kwa viwango vilivyokubaliwa. Vile vile, Taasisi hii ilianzishwa kufuatilia uwajibikaji na kurahisisha mawasiliano kati ya viongozi wa Serikali na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa miradi, changamoto zilizopo na mapendekezo ya namna ya kuzitatua. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi hii imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo itakayogharimu TZS 1.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Programu Shirikishi ya Maendeleo kwa Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar**

(Early Childhood Development (**ECD**) Programu ina lengo la kuhakikisha kuwa watoto wapatao 276,739 wa Zanzibar wanapata huduma za malezi bora kupitia utekelezaji wa Programu Shirikishi ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto (ZM-ECDP) kwa kuzingatia afya, lishe, elimu ya awali na ulinzi. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 1.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kukamilisha Moduli ya "ECD" ambayo inakwenda kujumuishwa katika Mtaala wa watoa huduma kwa makuzi ya watoto;
ii. Kutoa mafunzo yanayohusiana na "ECD" kwa watoa huduma za kiafya ngazi ya jamii Unguja na Pemba;
iii. Kuandaa Programu/Mpango wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto – Zanzibar;
iv. Kuandaa mpango wa utetezi (advocacy plan) kwa upande wa "ECD" na kuifanyia kazi; na
v. Kuweka vifaa vya michezo na kujifundishia katika vituo vya watoto kimoja Unguja na Kimoja Pemba.

## 7.2 Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Ofisi hii ina jukumu la kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja ikiwemo kukuza na kushajihisha uwekezaji wa ndani na nje, kuimarisha uwezo wa ujasiriamali, kutafuta upatikanaji wa kazi za staha kwa kuzingatia Sheria na viwango vya kazi. Sekta hii inatekeleza shughuli zake kupitia Mipango na Mikakati ya Kimaendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo kwa gharama ya TZS 15.00 bilioni

**Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yote yaliyoainishwa kwa uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ujenzi wa barabara za Zone "B" Micheweni; na
ii. Uwekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la uwekezaji Fumba.

### 7.2.1 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar

Taasisi hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuongeza ajira kwa vijana na wajasiriamali, pamoja na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa kwa wafanyabiashara nchini. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 10.60 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.10 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali Wadogo, Wakati na Wakubwa kwa kuwapatia mikopo itakayowasaidia kuongeza mitaji yao ili waweze kujitegemea. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Abudhabi kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.60 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.10 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Kutoa mikopo kwa wajasiriamali, wazalishaji wadogo, wakati na wakubwa.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kutoa mikopo kwa wafanyabiashara, wazalishaji na wajasiriamali (wadogo, wakati na wakubwa); na
ii. Kuratibu na kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

***Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)***

Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na kuwezesha vikundi vya kijamii kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kukuza masoko ya bidhaa. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara.

## 7.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ina jukumu la kutafuta, kudhibiti na kusimamia rasilimali fedha ili kuwezesha maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Ofisi pia ina jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato kutokana na kodi, ushuru na vyanzo vingine pamoja na kudhibiti Taasisi za kifedha zikiwemo benki kuweka utulivu wa kifedha na usalama wa amana za wananchi. Ofisi hii inawajibu wa kuandaa na kutekeleza sera za kifedha zinazochochea ukuaji wa Uchumi, kuimarisha mzunguko wa fedha na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepangiwa kiasi cha TZS 686.27 bilioni (TZS 649.10 bilioni kutoka Serikalini na TZS 37.17 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya kuteleza programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo.

### Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar

Programu hii ina lengo la kujenga na kukarabati majengo ya Ofisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa utendaji kazi wa Taasisi na Idara za Serikali unakuwa bora, na pia kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi Serikalini yanayokwenda sambamba na utoaji huduma nzuri kwa wananchi. Programu inajumuisha ujenzi wa Ofisi mpya za Serikali katika maeneo yaliyotengwa ili kuhakikisha huduma za Serikali zinapatikana karibu na wananchi pamoja na kuimarisha majengo ya zamani ili yawe na usalama na kuendelea kutoa huduma. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 126.30 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa Taasisi za Serikali ikiwemo Mamalaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Shirika la Magazeti, Ofisi ya Nyaraka, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji na Chuo cha Utawala wa Umma;
ii. Kuanza ujenzi wa Taasisi za Serikali ikiwemo Baraza la Wawakilishi, Mamlaka ya Serikali Mtandao, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Ofisi ya Usalama wa Serikali na Ofisi ya Tume ya Utumishi Serikalini; na
iii. Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka.

### Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

Programu hii inalenga kuimarisha miundombinu, huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 32.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga vituo viwili vya kusafirishia taka na vizimba 125 vya kukusanyia taka kwa Unguja na Pemba;
ii. Kuendeleza maeneo ya utalii katika vijiji vya Nungwi, Chwaka na Makunduchi - Unguja;
iii. Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji kwa kuwapatia watendaji mafunzo ya muda mfupi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi;
iv. Kuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Kijiografia kwa kisiwa cha Pemba;
v. Kuandaa Mfumo wa Utambuzi wa Taarifa za Kijiografia;
vi. Kuandaa Kanuni za ujenzi Zanzibar;
vii. Kununua magari ya taka 26 (11 ya kushindilia taka na 15 ya kuchukulia taka) kwa ajili ya usafi wa mji; na
viii. Ujenzi wa mradi salama wa watembea kwa miguu katika eneo la Mji Mkongwe.

### Programu ya Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – VI)

Programu hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 4.75 bilioni (TZS 350.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 4.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi 50 kuhusu masuala ya ununuzi unaozingatia athari za mazingira (Green Procurement) na kuandaa Hadidu Rejea (ToR) na Maandiko ya Dhana za Miradi (Concept note) kwa wanufaika 15 wa miradi. na
ii. Kupata Mahitaji ya mifumo mitatu (ZGAMIS, ZAN MALIPO na PAYROLL SYSTEM).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

i. Kufanya mapitio ya Sheria, Sera na Kanuni zinazohusiana na mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi;
ii. Kuandaa utafiti wa mtazamo wa utumiaji wa mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki; na
iii. Kuwajengea uwezo watumishi kuhusiana na mageuzi ya fedha za umma.

***Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG)***

Mradi una lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili kupitia Sera na Sheria stahiki. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia TZS 50.00 milioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kutoa huduma za uratibu na usimamizi wa shughuli za mradi.

### 7.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ndiyo chombo cha juu chenye uwezo wa kupanga na kusimamia utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi na mipango ya huduma za jamii Zanzibar. Katika kutekeleza majukumu yake, Tume ya Mipango inaandaa Mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi. Kwa mujibu wa Sheria Nambari 3 ya mwaka 2012 Tume ya Mipango pia ina jukumu la kuratibu masuala ya tafiti na idadi ya watu. Aidha, Tume ina jukumu la kutathmini hali ya Uchumi na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza changamoto za kiuchumi na kijamii ikiwemo ukosefu wa ajira, kuratibu na kupanga vipaumbele vya nchi na kutoa miongozo ya kimaendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, Tume ya Mipango imepangiwa jumla ya TZS 12.80 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza programu moja na miradi mitatu ya maendeleo.

**Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara**

Programu hii inalenga kuinua hali za wananchi kupitia urasimishaji wa Ardhi na Biashara ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa masjala ya ardhi Chake Chake - Pemba;
ii. Ununuzi na uwekaji mfumo wa makabati ya kielektroniki kwa ajili ya kuhifadhia kumbukumbu na nyaraka za biashara na ardhi ;
iii. Kufanya tathmini ya wafanyabiashara wadogo wadogo;
iv. Kuendelea na kazi ya urasimishaji wa ardhi na uchapishaji na ugawaji wa hati za matumizi ya Ardhi;
v. Kuimarisha mfumo wa utambuzi wa ardhi; na
vi. Kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo Unguja na Pemba.

***Mradi wa Kuratibu, Kupanga na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo***

Mradi huu una lengo la kuratibu shughuli za upangaji na usimamizi wa rasilimali fedha zinazotengwa na kutolewa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Mradi pia una lengo la kuimarisha uwezo wa Wizara na Taasisi za Serikali ili ziweze kusimamia rasilimali fedha kwa ufanisi zaidi kwa kuweka mifumo ya uwazi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa TZS 5.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa Mpango Mpya wa Maendeleo wa muda wa kati (2026-2031) baada ya ZADEP kufikia mwisho wa utekelezaji wake Juni 2026;
ii. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya uendelezaji wa Mfumo Jumuishi wa Uratibu wa Mipango ya Maendeleo (ZiPS) pamoja na kujenga uwezo kwa watendaji wa Sekta/Taasisi za Serikali juu ya matumizi ya Mfumo;
iii. Kuratibu zoezi la uthamini na uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na
iv. Kufanya tafiti (study) za kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia makundi hatarishi.

***Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa***

Mradi huu unalengo la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika

2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Mradi unahusisha utekelezaji wa mifumo ya kufuatilia na kupima maendeleo ya miradi ya maendeleo ili kuona kama malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa vigezo vilivyowekwa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa TZS 1.80 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kushiriki mikutano ya Kimataifa kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo;
ii. Kuwajengea uwezo Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia;
iii. Kuandaa Mwongozo na Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango wa Maendeleo (2026-2031);
iv. Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E Framework) wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026–2031;
v. Kuandaa na kuchapisha Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa Zanzibar kwa mwaka 2025–2026; na
vi. Kuandaa nyenzo shirikishi ya ufuatiliaji wa viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango wa muda wa kati wa Maendeleo wa Zanzibar na Ajenda za Afrika 2063.

***Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati***

Mradi unalenga kukuza uwezo wa kitaasisi na kitaalamu katika kufanya tafiti zenye mwelekeo wa kimkakati, ambazo zitasaidia kutoa mapendekezo ya kisera, kubaini maeneo ya vipaumbele vya maendeleo na kusaidia katika uundaji wa mipango inayozingatia ushahidi. Mradi huu utaimarisha uratibu wa shughuli za utafiti na kuhakikisha matokeo yanatumika kwa tija katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo na unatarajiwa kuchochea ubunifu, kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, na kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika shughuli za utafiti. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa na kuchapisha Agenda ya Tafiti Zanzibar 2026-2031;
ii. Kuratibu na kufanya tafiti na ubunifu Zanzibar; na

iii. Kujenga uwezo juu ya kuandaa maandiko ya Utafiti, kuandika ripoti na kutumika "software" kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa taarifa za tafiti.

### 7.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni Taasisi yenye jukumu la msingi la ukusanyaji, uchambuzi, na utoaji wa takwimu za Taifa, ambazo hutumika katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ofisi hii inachukua jukumu pia la kutoa taarifa sahihi na za kuaminika zinazohusiana na hali ya uchumi, demografia, afya, elimu na maeneo mengine muhimu ya Taifa. Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na mradi mmoja. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepangiwa jumla ya TZS 6.92 bilioni (TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.91 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP-II)**

Programu ina lengo la kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar kwa kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati, kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia takwimu za kawaida, sensa na tafiti. Programu inalenga kuwezesha uzalishaji na usimamizi wa takwimu, uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, maendeleo ya rasilimali watu kwa Taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa takwimu rasmi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.60 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2025/2026;
ii. Kukusanya, kutayarisha na kutoa uchambuzi wa kizio cha Mfumko wa bei (Consumer Price Index);
iii. Kufanya Utafiti wa mwaka na robo mwaka wa uzalishaji viwandani;
iv. Kufanya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2023/2024;
v. Kukamilisha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS);
vi. Uwasilishwaji wa ripoti ya utafiti wa uwajiri na mapato; na
vii. Kufanya utafiti wa sekta zisizo rasmi.

*Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia*

Mradi una lengo la kuimarisha uzalishaji na matumizi ya takwimu za jinsia ambazo husaidia katika kubuni sera na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambayo inazingatia mahitaji na haki za jinsia hasa katika masuala ya elimu, afya, ajira na haki za kijamii. Vile vile, kutoa elimu ya dhana ya udhalilishaji wa kijinsia na aina zake, kutambua makundi au maeneo ambayo yako katika hatari zaidi ya udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.32 bilioni (TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 320.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuandaa warsha ya uhamasishaji kwa wazalishaji na watumiaji wa takwimu za jinsia;
ii. Kufanya vikao vya Kamati ya Kitaalamu ya takwimu za kijinsia na kuandaa mafunzo ya utatuzi wa dhana za jinsia;
iii. Kufanya utafiti katika Kaya kuhusu maswala ya udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar;
iv. Kutayarisha "dashboard" ya takwimu za kijinsia;
v. Kufanya ziara kwa ajili ya kujifunza takwimu za kijinsia; na
vi. Kutoa toleo la kila mwezi la takwimu za jinsia.

### 7.3.3 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali

Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni taasisi ya msingi katika kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na matumizi mazuri ya rasilimali za umma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za fedha za umma. Katika kutekeleza jukumu lake, Ofisi inashirikiana kwa karibu na taasisi nyingine za kifedha, Mamlaka za Serikali za mitaa, Wakaguzi wa nje na wa ndani, pamoja na Wadau wa maendeleo ili kuimarisha mnyororo wa usimamizi wa fedha za Serikali, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wa maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja utakaogharimu kiasi cha TZs 1.02 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL) kwa Viwango vya Kimataifa

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma kwa kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha zinawasilisha hali

halisi ya kifedha Serikalini. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.02 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kufanya mapitio ya Miongozo ya Kihasibu;
ii. Kutoa uelewa wa sera na miongozo ya uhasibu kwa wahusika Unguja na Pemba;
iii. Kuufanyia mapitio ya mfumo wa BAMAS na kuunganisha na mapato na mfumo wa usimamizi wa mali pamoja na kuimarisha moduli zilizomo ili ziendane na mfumo wa "Accrual";
iv. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na miundombinu pamoja na ununuzi wa samani na vitendea kazi vya Ofisi; na
v. Kukijengea uwezo kikosi kazi cha usimamizi wa mradi na kufanya warsha ya wadau kuhusiana na "Accrual".

### 7.4 Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi hii ina dhamana ya kuhakikisha uwepo wa utumishi wa umma wenye ufanisi na utakaotoa huduma bora kwa jamii kwa kuzingatia misingi ya haki, sheria, na demokrasia ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zinazoheshimu misingi ya haki za binadamu. Ofisi inasimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo inayohusiana na utawala bora kwa jamii ya Zanzibar, ili kuweka misingi ya uwajibikaji. Kwa mwaka 2025/2026 Ofisi imepanga kutekeleza Programu mbili na miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 7.22 bilioni (TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.72 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)*

Pragramu hii ina lengo la kuimarisha uwajibikaji na utendaji wa watumishi wa umma Zanzibar kwa kuzingatia taratibu zilizo bora zaidi katika utoaji wa huduma stahiki kwa jamii. Kwa mwaka 2025/2026. Programu imepangiwa kiasi cha TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kutayarisha Mfumo Ikama wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma (Norminal Roll);

ii. Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma;
iii. Kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa Ufuatiliaji Uwajibikaji wa Utawala Bora katika Taasisi za Umma; na
iv. Kuanzisha Mfumo wa kusimamia taarifa za watumishi (Employee Management System).

**Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria**

Programu ina lengo la kuwezesha wananchi kisheria pamoja na kuimarisha upatikanaji haki kwa wote. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kiasi cha TZS 1.73 bilioni (TZS 500 milioni kutoka Serikalini na TZS 1.23 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo)

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuanzisha Mfumo wa kielektroniki wa kupitia Mikataba kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu (AGCMIS - Attorney General's Chamber Management Information System); na
ii. Kuanzisha Mfumo wa usajili na usimamizi wa Watoa huduma za kisheria (Legal Aid Providers Management Information System - LAPMIS).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuimarisha mifumo na uwezo wa Taasisi za Sheria na rasilimali watu;
ii. Kuziwezesha Asasi za Kiraia kutoa msaada wa kisheria na kuhamasisha jamii juu ya haki za kisheria na za kibinadamu kwa makundi hatarishi; na
iii. Kuanzisha utaratibu wa kuelimisha jamii juu ya huduma ya haki katika kesi za unyanyasaji wa kijinsia.

**Mradi wa Utoaji wa Huduma ya Haki kwa Kuzingatia Jinsia**

Mradi huu una lengo la kutoa huduma za haki kwa wanawake na wasichana ili kuwasaidia kukabiliana na kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 143.31 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha mazingira wezeshi yatakayokuza mfumo wa kisheria na kisera wa kukabiliana na kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na watoto Zanzibar; na
ii. Kuimarisha uwezo wa uratibu wa sekta mbali mbali ili kuzuia na kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

***Mradi wa Kujenga Msingi Imara wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Tanzania***

Mradi huu una lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu madhara ya rushwa pamoja na kukuza ushirikiano kati ya Taasisi za umma, Sekta binafsi, na jamii katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa. Kwa upande wa Zanzibar mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 4.34 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha usimamizi na ubora wa taarifa zinazowasilishwa kwa wachunguzi;
ii. Kuimarisha mfumo wa haki jinai kwa watuhumiwa, waathiriwa, na mashahidi katika kulinda haki zao;
iii. Kuimarisha uongozi wa Taasisi mbali mbali katika usimamizi wa taarifa za kiutawala; na
iv. Kuongeza uwezo wa mfumo wa haki ya jinai Zanzibar katika kutambua na kusimamia mali kwa mujibu wa taratibu.

### 7.4.1 Mahkama Kuu

Ofisi hii ina jukumu la kupokea, kusikiliza, kutoa maamuzi, mashauri ya jinai na madai yaliyowasilishwa mahkamani, ili kuhakikisha upatikanaji wa haki nchini. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 48.60 bilioni (TZS 13.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Wilaya na Mikoa***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwa na Mahkama za kisasa zenye mazingira mazuri pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Kwa mwaka 2025/26, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 13.00 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Mazizini;
ii. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Wilaya ya Magharibi "B" katika eneo la Kisakasaka;
iii. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini katika eneo la Pale - Unguja;
iv. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Tunguu/Binguni;
v. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Kinyasini;
vi. Kuendelea na ujenzi Mahkama ya Wilaya ya Micheweni Pemba katika eneo la Micheweni; na
vii. Kuendelea na ujenzi wa Mahkama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Mfikiwa Chake – Chake.

*Mradi wa Uimarishaji wa Mahkama*

Mradi una lengo la kuimarisha Mahkama katika kuwezesha upatikanaji wa haki pamoja na kuongeza ufanisi kwa watendaji wa Mahkama. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 35.60 bilioni (TZS 600 milioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

i. Ununuzi wa samani kwa majengo ya Mahkama;
ii. Ununuzi wa kompyuta na vifaa vyake; na
iii. Ununuzi wa huduma za kimtandao.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

i. Ujenzi wa majengo ya Mahkama za Wilaya (Kijichi, Makunduchi, Chwaka, Kinduni na Kigunda);
ii. Ukarabati wa majengo ya Mahkama ya Mahonda na Wete;
iii. Kulipa ada ya Mshauri Elekezi; na
iv. Kufanya mafunzo ya kujenga uwezo wa utekelezaji na usimamiaji wa miradi kwa watumishi.

## 7.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kuhakikisha kuwa Mikoa na Serikali za Mitaa zinafanya kazi kwa ufanisi na kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za nchi. Vile vile, Wizara inaratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi za Mikoa na Serikali za mitaa na Idara Maalum za SMZ ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na miradi sita ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 92.12 bilioni (TZS 81.75 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi***

Programu ina lengo la kuimarisha mifumo ya Serikali katika kutekeleza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuongeza uwekezaji katika miradi ya mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya jamii na kuimarisha uwezo wa Serikali kuu kuweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yaliyo hatarini zaidi. Programu inatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa kiasi cha TZS 2.10 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa miongozo ya usimamizi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi;
ii. Kuzijengea uwezo Halmashauri juu ya uendeshaji na usimamizi wa miradi;
iii. Kujenga uwezo wa Kitaasisi, wafanyakazi na kutoa elimu kwa jamii; na
iv. Uratibu wa shughuli za mradi.

***Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama***

Mradi una lengo la kuimarisha usalama wa jamii kwa kuhakikisha kuwa kuna miundombinu ya kisasa ya ulinzi na usalama ikiwemo uwekaji wa mifumo na vifaa vya kisasa vya ulinzi ili kulinda wananchi na mali zao dhidi ya uhalifu na viashiria hatarishi. Kwa kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mikakati ya ulinzi na usalama mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali, kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25.75 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa vituo vya ufuatiliaji wa matukio ya "CCTV" eneo la Maisara -Unguja, kwa upande wa Pemba - Chake Chake, Wete na Mkoani;
ii. Kufanya matengenezo ya kamera za ulinzi na usalama (mfumo mzima wa CCTV);
iii. Ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya Idara Maalum za SMZ;
iv. Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya kiulinzi katika Idara Maalum za SMZ;
v. Kukarabati jengo la Ofisi ya mradi eneo la Maisara;
vi. Kuimarisha mafunzo na vifaa vya kiutendaji kwa Wakala wa Ulinzi, askari na vijana wa JKU;
vii. Kuimarisha miundombinu na mazingira ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo.

***Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar***

Mradi una lengo la kuratibu shughuli mbali mbali za Serikali na kijamii kama vile usajili wa vizazi na vifo, uidhinishaji wa nyaraka na utoaji wa taarifa muhimu kwa wananchi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 8.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa Ofisi za Masheha kwa Shehia 130 Unguja na Pemba; na
ii. Ununuzi wa samani za Ofisi za Masheha kwa Shehia 130.

***Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai***

Mradi una lengo la kubadilisha tabia za watoto na vijana kwa kuwapa msaada unaohitajika kupitia Chuo cha Marekebisho ya Tabia ili kubadilisha tabia zao na kuweza kurejea katika jamii wakiwa raia wema na kuweza kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Mradi unalenga kuhakikisha kuwa haki jinai inapatikana kwa wote na kuwa na mfumo wa haki unaozingatia usawa, haki na ufanisi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 18.00 bilioni.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa majengo ya kisasa ya Chuo cha Kurekebisha Tabia cha Hanyegwa mchana.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe***

Mradi una lengo la kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika eneo la Mwanakwerekwe, kuhakikisha kuwa kuna mazingira bora na salama kwa ajili ya maegesho ya magari kwa usafiri wa umma na binafsi, pamoja na kuongeza ufanisi wa shughuli za kibiashara katika soko hilo. Pia, kuweka mazingira mazuri kwa watumiaji wa soko na utoaji wa huduma za kijamii. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 20.00 bilioni.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza ujenzi wa kituo cha dalalada na maegesho ya vyombo vya usafiri katika eneo la Mwanakwerekwe.

***Mradi wa Kijani - Pemba***

Mradi una lengo la kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, mifumo ya maji safi na taka, kuwa na maeneo ya kijani ya bustani na viwanja vya michezo. Kuiweka miji katika mazingira safi, salama na yenye kuvutia kwa wakaazi na wageni pamoja na kuwezesha miji kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia teknolojia endelevu na mbinu rafiki kwa mazingira. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 8.27 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukarabati wa masoko mawili Chake Chake na Mkoani Pemba;
ii. Ujenzi wa miundombinu ya usafishaji katika vituo vya huduma za afya Chake Chake na Mkoani Pemba;
iii. Kuimarisha Kamati za usimamizi na kuongeza elimu ya utumiaji wa fursa za masoko pamoja na shughuli za kibiashara katika soko la Wete na Micheweni;
iv. Ukarabati wa viwanja vya michezo eneo la Jadida, Mitiulaya, Micheweni na kuimarisha uhifadhi wa mazingira eneo la bustani ya Jamhuri – Wete;
v. Kuongeza uwezo wa utoaji huduma za kijani eneo la msitu wa Ngezi-Vumawimbi;

vi. Ujenzi wa vituo vya kuchomea taka za Hospitali katika vituo vitano vya afya;
vii. Ununuzi wa vifaa na kuimarisha vikundi vya ukusanyaji taka Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba;
viii. Kuanzisha Mifumo ya kukusanya maji ya mvua, kufanya matengenezo ya visima na kuimarisha huduma ya maji safi na salama eneo la Wete na Mkoani;
ix. Kufanya ukarabati wa vituo vya mabasi na kazi za kuunganisha maeneo ya kijamii ili kuweza kufikika kwa kutumia barabara za ndani eneo la Mji wa Chake Chake;
x. Kufanya ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira kwa Skuli za msingi za Madungu, Shamiani, Ng'ombeni 'A' na 'B';
xi. Ukarabati wa visima viwili eneo la Weni na Kizimbani Pemba;
xii. Kufanya utafiti kuhusiana na uwezo wa kiuchumi kwa vikundi vya wanawake na vijana kwa kuzingatia fursa za biashara ndogo ndogo za kijani;
xiii. Kutoa huduma na elimu juu ya athari zinazohusiana na usimamizi na uteketezaji wa taka katika skuli ya Jadida na Micheweni; na
xiv. Kuimarisha vikundi vya wanawake na vijana kwa maendeleo ya biashara ndogo ndogo kwa kuanzisha biashara mpya na kuzikuza zilizopo.

***Mradi wa Mji Bila Taka***

Mradi una lengo la kuimarisha mazingira na afya ya jamii, kuzuia utupaji ovyo wa taka na kuhakikisha kuwa taka zinakusanywa na kutupwa kwa njia sahihi. Kusimamia usafishaji wa Miji na kuhakikisha miji inasafishwa na kuweka vifaa vya kutosha vya kuhifadhia taka. Pia, mradi unaendesha kampeni za uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira na jinsi ya kushiriki katika shughuli za kuzuia uchafuzi wa mazingira. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 10.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha miundombinu ya Miji ikiwemo mitaro, njia za watembea kwa miguu na taa za barabarani;
ii. Kupendezesha Miji kwa kupanda miti na bustani katika maeneo ya wazi; na

iii. Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi taka na vifaa kwa ajili ya udhibiti wa taka ngumu.

### 7.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kusajili na kutoa vyeti kwa matukio muhimu ya kijamii ikiwemo: kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka pamoja na utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 3.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii***

Mradi una lengo la kuimarisha mifumo ya usajili ili takwimu za matukio ya kijamii ziwe sahihi na zinapatikana kwa wakati. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 1.50 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuingiza kumbukumbu za vizazi hai ndani ya mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii na takwimu zake;
ii. Kuimarisha mfumo wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi; na
iii. Ujenzi wa kituo cha urejeshaji wa huduma baada ya majanga (Disater Recovery Center).

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii***

Mradi una lengo la kuweka miundombinu ili kuimarisha utoaji wa huduma. Vituo vya utoaji wa huduma za jamii katika maeneo ya mijini na vijijini vitaimarishwa ili kuhakikisha huduma zinapatikana kwa urahisi kwa wananchi wote. Vile vile, kuimarisha mtandao kwa Ofisi zote za usajili ili kuwezesha mawasiliano na ushirikiano bora kati ya Ofisi zao na Makao Makuu. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 2.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Usajili Wilaya ya Kaskazini B - Mahonda; na
ii. Kuimarisha shughuli za mifumo na ununuzi wa gari mbili za Ofisi.

### 7.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina lengo la kudhibiti na kuzuia magendo ya bahari, kulinda usalama wa nchi, kupambana na magendo na kuimarisha uchumi wa bahari kupitia uvuvi wa kisasa. Aidha, kikosi kinatekeleza juhudi za Serikali katika kuinua uchumi wa buluu kupitia uvuvi wa bahari. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 5.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM***

Mradi una lengo la kuimarisha utendaji kazi na makaazi ya maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ ili wawe na mazingira mazuri ya kazi. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umetengewa kiasi cha TZS 2.50 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa Makao Makuu - Kibweni; na
ii. Ujenzi wa mahanga katika Kambi ya Bwefum.

***Mradi wa Kuimarisha Shughuli za Uzamiaji na Uokozi***

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi na uokozi baharini kwa kutoa huduma za uzamiaji na uokozi pale yanapotokezea maafa ya baharini yanayosababishwa na majanga ikiwemo kuzama kwa vyombo vya baharini, vyombo vya abiria na mizigo kwa Unguja na Pemba. Mradi unatekelezwa kupitia fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2025/2026 umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza na ujenzi wa Kituo cha Uzamiaji na Uokozi Wete - Pemba na Kizimkazi – Unguja;
ii. Ununuzi wa meli ya "landcraft"; na
iii. Ununuzi wa vifaa vya uzamiaji na uokozi.

### 7.5.3 Kikosi cha Valantia

Kikosi kina lengo la kutoa huduma ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Taasisi nyengine za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Kikosi kina kazi ya kudumisha amani na mshikamano wa Taifa kwa kutekeleza sera na mipango ya

kuleta maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepangiwa kiasi cha TZS 5.52 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari***

Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuwa na Idara Maalum za SMZ zenye majengo mazuri yatakayoimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.52 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa bohari mbili za kuhifadhia vifaa Makao Makuu Mtoni -Unguja na Ndugukitu - Pemba;
ii. Kuendelea na majengo ya utoaji huduma katika kambi ya Makao Makuu - Mtoni; na
iii. Kuanza ujenzi wa uwanja wa mpira katika kambi ya Mtoni.

### 7.5.4 Chuo Cha Mafunzo

Chuo Cha Mafunzo kina lengo la kukuza maadili mema, nidhamu na uwajibikaji kwa wanafunzi ili kuwa raia wema na viongozi bora wa baadae, kutoa elimu ya kivitendo na ujuzi kwa wanafunzi ili kuwawezesha kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu mbali mbali katika taaluma zao, pia chuo cha mafunzo kinajukumu la kuwaandaa vijana na soko la ajira na kuwawezesha kujiajiri. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepangiwa kiasi cha TZS 3.58 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga***

Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika makaazi mazuri. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.58 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa nyumba za ghorofa mbili (G+2) kambi ya Langoni na Hanyegwa Mchana - Unguja; na
ii. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa Makao Makuu Unguja.

### 7.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)

Jeshi lina lengo la kutoa mafunzo ya kiufundi, elimu ya sekondari na programu za uzalishaji kwa vijana. Vile vile, jeshi linalenga kuimarisha uwezo wa vijana na kuwaandaa kushiriki katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi cha JKU kimepangiwa kiasi cha TZS 14.53 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU***

Mradi una lengo la kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ kwa kuwapatia majengo yenye viwango stahiki. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.99 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano (G+5) la Makao Makuu ya JKU - Saateni;
ii. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makaazi ya watumishi wa JKU Ng'ambwa Pemba; na
iii. Kujenga Mahanga sita (Upenja, Kama na Dunga).

***Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia***

Mradi una lengo la kutoa huduma ya malazi kwa wanafunzi wanaoishi mbali na maeneo yao ya makaazi. Dakhalia itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu na kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya unyanyasaji. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.13 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi wa skuli ya JKU Mtoni.

***Mradi wa Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU***

Mradi una lengo la kuimarisha uwezo wa kulinda raia na mali zao katika maeneo tofauti ikiwemo taasisi za Serikali, biashara na makaazi binafsi. Aidha, mradi una lengo la kuongeza idadi na ufanisi wa walinzi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.42 bilioni.

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa*

- Kuanza ujenzi wa ghorofa mbili Makao Makuu ya Wakala wa Ulinzi JKU Mtoni.

### 7.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kikosi kina jukumu la kutoa huduma za haraka na za kitaalamu katika kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao. Vile vile, kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuhusu njia bora za kuzuia matukio ya ajali za moto na jinsi ya kukabiliana na majanga. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 25.76 bilioni.

***Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari***

Mradi huu una lengo la kuimarisha makaazi mazuri kwa askari wake ambapo mazingira hayo yatawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, mradi pia utapunguza changamoto za makaazi kwa maaskari na kuongeza hamasa katika kazi zao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Kilimani;
ii. Kukamilisha ujenzi wa Ofisi Kuu Chanjaani - Pemba; na
iii. Ujenzi wa Kituo cha zimamoto na uokozi Finya - Pemba.

***Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto***

Mradi una lengo la kuimarisha uwezo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kuhakikisha kuwa kuna vifaa vya kisasa na vya kutosha ili kuokoa maisha na mali za wananchi pindi inapotokezea ajali ya moto na majanga mengine. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 22.76 bilioni (TZS 2.55 bilioni kutoka Serikalini na TZS 20.21 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Ununuzi wa gari mbili na vifaa vya kutolea huduma za uokozi na uzimaji moto.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ununuzi wa vifaa na magari ya utoaji huduma za uokozi na uzimaji moto;

ii. Ununuzi wa boti za uokozi kwa maeneo ya visiwa vidogo vidogo; na
iii. Kutoa mafunzo kwa wapiganaji.

### 7.6 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Ofisi ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa maeneo mtambuka ikiwemo mazingira, watu wenye ulemavu, Ukimwi na udhibiti wa madawa ya kulevya. Ofisi hii imepewa dhamana ya kuhakikisha mshikamano wa kitaifa, ushirikiano wa kisera na kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepangiwa kutekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 5.91 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.41 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

Programu hii ina lengo la kuziwezesha Serikali za Mitaa kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia TZS 598.22 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa miongozo na vitini vya kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi kwa Serikali za Mitaa;
ii. Kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa na jamii juu ya uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yao; na
iii. Kuandaa mfumo wa kuripoti taarifa za athari za mabadiliko ya tabianchi kwa Unguja na Pemba.

Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira Mradi umeanzishwa kwa lengo la kutathmini na kusaidia kupunguza athari za maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuchukua hatua mahsusi za kudhibiti na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa ukuta wa kuzuia athari katika maeneo ya makaazi na mashamba; na
ii. Kufanya zoezi la kutathmini na usimamizi wa athari za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani
Mradi una lengo la kuwajengea uwezo wakulima wadogo wadogo katika maeneo yenye miradi hiyo kuweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza tija zaidi katika uzalishaji. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia TZS 815.22 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutoa mafunzo kwa wanajamii juu ya uendeshaji na matengenezo ya bwawa la kuvunia maji ya mvua;
ii. Uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika maeneo yote ya mradi pamoja na kuanzisha Jumuiya za umwagiliaji;
iii. Kuwasaidia wakulima kuanzisha shamba darasa na kilimo cha majaribio katika ardhi ya chumvi;
iv. Kurejesha uoto wa asili katika maeneo yalioathirika kwa kupanda miti;
v. Ujenzi wa matuta kwa eneo la Bumbwini Mafufuni na Kiongwe kidogo Unguja;
vi. Ujenzi wa visima na makinga maji eneo la Tovuni - Pemba;
vii. Utoaji wa mtaji, vifaranga vya kuku na vifaa kwa wafugaji katika eneo la mradi;
viii. Kukuza uwelewa wa jamii juu ya usimamizi wa pamoja wa vyanzo vya maji;
ix. Ununuzi wa mizinga na mashine za kusarifu asali kwa maeneo ya mradi; na
x. Kutoa mafunzo pamoja na kusaidia jamii juu ya uanzishaji wa vitalu vya mikoko na miti mengine.

### 7.6.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni Taasisi iliyoanzishwa kisheria na kupewa jukumu la kuhakikisha mazingira ya Zanzibar yanatunzwa, yanahifadhiwa na yanaendelezwa kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kurithisha kizazi kijacho. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi imepangiwa jumla ya TZS 1.15 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 152.10 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutetekeleza programu moja na mradi mmoja wa maendeleo.

**Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

Programu hii ina lengo la kuziwezesha Serikali za Mitaa kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia TZS 152.10 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha mfumo wa kudhibiti na kufuatilia athari za kimazingira na kijamii ili kusaidia hatua za uhimili wa mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya zilizochaguliwa; na
ii. Kufanya mafunzo ya tathmini na ufuatiliaji wa athari za kimazingira kwa Mamlaka na Serikali za Mitaa Unguja na Pemba.

***Mradi wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani***

Mradi huu una lengo la kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kuelewa umuhimu wa kuhifadhi miti na misitu iliyopo, kupanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukuza uelewa juu ya utekelezaji wa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani;
ii. Kuimarisha vitalu kwa ajili ya upatikanaji wa mbegu na miche kutoka Serikalini na Taasisi binafsi;
iii. Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na vitendea kazi; na
iv. Kuimarisha zoezi la ufuatiliaji na tathmini.

### 7.6.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya Zanzibar ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kuratibu, kusimamia na kutekeleza mikakati ya kupambana na matumizi na usambazaji wa madawa ya kulevya ndani ya Zanzibar. Hii ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kulinda afya ya jamii, kuimarisha usalama wa raia na kupunguza athari mbaya za madawa ya kulevya kwa vijana na jamii kwa ujumla. Kwa mwaka 2025/2026, Mamlaka imepangiwa kutekeleza mradi mmoja wenye jumla ya TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya***

Mradi huu una lengo la kutoa tiba na marekebisho ya tabia kwa wanaotaka kuachana na matumizi ya dawa za kulevya. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia – Pemba; na
ii. Ununuzi wa vitendea kazi pamoja na vifaa vya maabara.

**7.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi**

Ofisi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sambamba na kuratibu masuala ya Muungano (Zanzibar na Tanzania bara) kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kulinda haki za binadamu na ushirikishwaji wao. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na miradi miwili itakayogharimu jumla ya TZS 37.65 bilioni (TZS 2.65 bilioni kutoka Serikali TZS 35.00 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo).

**Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III)**

Programu inatekelezwa kwa lengo la kuziwezesha Kaya zenye kipato cha chini sana kuongeza vipato vyao, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika elimu, afya na ajira za muda mfupi. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kiasi cha TZS 35.10 bilioni (TZS 100.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo)

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuratibu shughuli za TASAF Unguja, Pemba na Tanzania bara;
ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi wa TASAF; na
iii. Kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ujenzi wa dakhalia ya wavulana na uzio wa kuzunguka dakhalia la wasichana katika Skuli ya Kizimkazi Dimbani;
ii. Ujenzi wa uzio katika kituo cha afya Donge Vijibweni na Uzi Ng'ambwa; na
iii. Kuhaulisha fedha kwa Kaya za walengwa wa TASAF.

*Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais*

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wafanyakazi ili kuwa na makaazi yanayoendana na nyadhifa zao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Iliopangwa kutekelezwa.*

- Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais katika eneo la Tibirinzi Chake Chake - Pemba.

*Mradi wa Ukarabati wa Ofisi ya Uratibu Dar-es-salaam*

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wafanyakazi wake Dar-es-Salaam. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 550.00 milioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa.*

i. Ukarabati wa jengo la Ofisi ya Uratibu - Dar es Salaam; na
ii. Ujenzi wa njia, maeneo ya bustani na maegesho katika eneo la Ofisi ya uratibu Dar-es-Salaam.

## 7.8 Wizara ya Afya

Wizara ya Afya ina jukumu la kusimamia afya za wananchi kwa kuhakikisha huduma za kinga na tiba zinapatikana pamoja na kutoa maelekezo ya kitaalamu juu ya afya ili kuwa na jamii yenye afya bora. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu kumi na miradi mitatu ya maendeleo yenye thamani ya jumla ya TZS 188.24 bilioni (TZS 83.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 104.79 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar

Programu hii ina lengo la kutokomeza maradhi ya malaria hapa Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 7.27 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.27 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

i. Utumiaji wa taarifa na ufuatiliaji wa wagonjwa hospitalini, vituoni na majumbani;
ii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria; na
iii. Uratibu na usimazi wa uendeshaji wa shughuli za malaria.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

i. Utumiaji wa taarifa na ufuatiliaji wa wagonjwa hospitalini, vituoni na majumbani;
ii. Kuimarisha uchunguzi na matibabu ya ugonjwa wa malaria katika hospitali na vituo vya afya;
iii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria;
iv. Uratibu na usimazi wa uendeshaji wa shughuli za malaria; na
v. Uthibiti wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria.

**Programu ya Kudhibiti Maradhi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma**

Programu hii ina lengo la kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi ya kifua kikuu, homa ya Ini na kupunguza maambukizi ya Ukoma. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 5.85 bilioni zimetengwa kutekeleza programu hii (TZS 4.85 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

i. Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu na makundi maalum wanaoishi na VVU;
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya homa ya ini katika jamii;
iii. Uhamasishaji na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, magonjwa ya kujamiana, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma;
iv. Uratibu na usimamizi wa kazi za programu ya huduma shirikishi ya homa ya ini, ukimwi, kifua kikuu na ukoma;
v. Kufanya uhamasishaji kwa wanaume juu ya upimaji wa virusi vya ukimwi wakati wa mahudhurio ya kliniki; na
vi. Kuimarisha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu wa makundi maalum wanaoishi na VVU;
ii. Uhamasishaji na kuongeza uelewa katika jamii juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, magonjwa ya kujamiana, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma;
iii. Uratibu na usimamizi wa kazi za programu ya huduma shirikishi ya homa ya ini, Ukimwi, kifua kikuu na ukoma; na
iv. Kuimarisha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

**Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

Programu hii ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 6.28 bilioni zimetengwa (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.28 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuimarisha matibabu jumuishi ya watoto chini ya miaka mitano pamoja na kuimarisha miongozo ya matibabu ya watoto;
ii. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano na wachanga;
iii. Uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya mama na mtoto;
iv. Kutoa elimu kwa vijana juu ya athari za mimba za utotoni;
v. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto; na
vi. Kuimarisha huduma za damu salama kwa mama wajawazito na watoto.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ukarabati wa vituo vya afya kwa vijana, ununuzi wa chanjo, dawa na vifaa tiba;
ii. Kufanya majadiliano kwa jamii juu ya wajibu wao katika huduma za uzazi wa mpango;
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto;
iv. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo ya mama na mtoto;

v. Uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya mama na mtoto;
vi. Ukarabati na uwekaji wa vifaa vituo vya mkono kwa mkono vitakavyosaidia kujikinga na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika Mikoa mitatu;
vii. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano na watoto wachanga; na
viii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto.

**Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto**

Programu ina lengo la kuimarisha huduma za afya ya Msingi kwa mama na mtoto. Programu inatekelezwa na Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 25.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha miundombinu ya afya ya mama na mtoto;
ii. Ununuzi wa dawa na vifaa tiba vya huduma ya afya ya mama na mtoto;
iii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa programu;
iv. Ujenzi wa vituo vya afya ya msingi; na
v. Kusomesha Madaktari wa fani maalum.

**Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia utoaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 72.35 bilioni (TZS 35.35 bilioni kutoka Serikalini TZS 37.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i Kuanzisha Taasisi ya Afya ya Jamii - Binguni;
ii Kuendelea na ujenzi wa hospital ya wagonjwa wa afya ya akili eneo la Pandani - Pemba;
iii Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa katika eneo la Makunduchi na Mahonda;
iv Ujenzi wa Hospitali ya Saratani – Binguni;
v Ujenzi wa kituo cha kudhibiti sumu - Tunguu;
vi Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu Pemba;

vii Ujenzi wa Maabara katika Mamlaka ya Dawa, Chakula na Vipodozi Chamanangwe Pemba;
viii Kutekeleza Mradi wa 'Electronic Health Network';
ix Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba; na
x Kuimarisha mifumo ya kidigitali kwa afya katika ngazi zote.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i Kuwezesha ujenzi wa hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili Pemba;
ii Ujenzi wa hospitali ya Mkoa katika eneo la Makunduchi;
iii Ujenzi wa jengo la huduma za mama na mtoto hospitali ya Mkoa katika eneo la Mahonda; na
iv Ujenzi wa Hospitali ya Saratani – Binguni.

**Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi**

Programu hii ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii inatekelezwa na Serikali na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 20.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Ujenzi wa Vituo vya Afya 35 vya Dispensary-MEHECO; na
ii) Ujenzi wa vituo 18 vya afya ya Msingi.

**Programu ya Jamii ni Afya**

Programu hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwapelekea wahudumu wa afya katika ngazi ya Shehia ili jamii waweze kusaidia wananchi huduma za awali wanapopata matatizo ya kiafya. Programu inatekelezwa na Serikali na kwa mwaka 2025/2026, imepanga kutumia jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Kuongeza idadi na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ya jamii;
ii) Uratibu wa shughuli za wahudumu wa afya ya jamii; na
iii) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa kazi za wahudumu wa afya wa jamii.

**Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya – Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kuwasaidia wananchi wasiojiweza na makundi maalumu ikiwemo wazee kuanzia miaka 65, wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano na wenye hali ya kipato cha chini (Masikini) kwa lengo la kupata huduma za afya kupitia mfuko wa huduma za afya ya Zanzibar ili kuhakikisha hakuna mwananchi aneachwa nyuma katika kupata kuduma za afya. Kwa mwaka 2025/2026, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 1.53 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 528.80 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuimarisha huduma za afya kwa watu wasiojiweza na makundi maalumu katika jamii.

**Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa**

Mradi una lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili wawe na utulivu wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi na kuwawezesha watoa huduma kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 3.00 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini.

**Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa**

i. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Wilaya Mbuzini; na
ii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Mkoa Mahonda.

**Programu ya Kuimarisha Nguvukazi**

Programu hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa madaktari bingwa na bobezi ili kuimarisha huduma za matibabu katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Rufaa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kusomesha madaktari bingwa.

***Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.40 bilioni (TZS 14.40 kutoka Serikalini na TZS 10.00 kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Ukarabati na utanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmmoja.

***Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya rufaa na kuimarisha miundombinu ya kufundishia taaluma za Afya. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.56 bilioni (TZS 1.700 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa majengo ya hospitali ya Binguni; na
ii. Ufuatiliaji na usimamizi wa ujenzi katika hospitali ya Binguni.

***Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali***

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa taarifa za afya na kuhakikisha taarifa zote za afya zinapatikana kwenye mfumo mama wa taarifa ili ziweze kutumika katika utungaji wa sera, uandaaji wa miongozo na ufanyaji wa maamuzi katika ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi kwa lengo la kupunguza vifo na kukabiliana na maradhi ya miripuko. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA kwenye vituo vya afya;
ii. Kutoa mafunzo kwa wasimamizi na watumiaji wa mifumo; na
iii. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA.

## 7.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuhakikisha kuwa ardhi inatumiwa kwa njia endelevu, kuepuka migogoro na matumizi mabaya ya yanayoweza kuathiri mazingira na maendeleo ya kijamii sambamba na utoaji na uendelezaji wa nyumba na makazi kwa wananchi. Wizara inaratibu sekta ya makaazi ambayo inahusisha ujenzi wa miji na makazi yanayokidhi viwango vya kisasa vya miundombinu na kuweka mazingira mazuri ya kuishi, ikiwa ni pamoja na huduma za jamii, usalama, na mazingira ya afya. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara hii imepanga kutumika kiasi cha TZS 335.69 bilioni kutoka Serikalini kwa utekelezaji wa programu mbili za maendeleo.

### Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo

Programu hii ina lengo la kujenga nyumba za kisasa na bora ili kukidhi mahitaji ya makazi, hasa katika maeneo yenye ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya nyumba. Programu pia ina lengo la kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa makazi. Programu inatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 300.12 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za bei nafuu Chumbuni na maeneo mengine;
ii. Ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara Mkungu Malofa - Chake Chake, Wete - Pemba na Nyamanzi - Unguja;
iii. Ujenzi wa nyumba 209 za makaazi Saateni; na
iv. Ujenzi wa mji mpya wa Kisakasaka 'A' na 'B' Unguja.

### Programu ya Upangaji wa Miji na Usimamizi wa Ardhi

Programu ina lengo la kuboresha na kupanga matumizi ya ardhi katika maeneo ya miji ili kuhakikisha maendeleo endelevu, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira. Programu hii itasaidia kuendeleza miji kwa njia inayozingatia ufanisi, usawa na matumizi bora ya rasilimali za ardhi. Upangaji wa miji na usimamizi wa ardhi ni muhimu katika kuhakikisha kuwa miji inakuwa na maendeleo endelevu, ina miundombinu bora na inatunza mazingira kwa vizazi vijavyo. Programu inatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 35.57 bilioni.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kufanya utambuzi kwa maeneo 150,000 (Unguja 100,000 na Pemba 50,000);
ii. Kuandaa mipango miji kwa Mkoa wa Mjini Magharibi; na
iii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa Ardhi.

**7.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda**

Wizara ina lengo la kukuza viwanda vidogo vidogo na vya kati sambamba na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu moja na mradi mmoja kwa gharama ya TZS 46.36 bilioni kutoka Serikalini.

**Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati katika maeneo ya Dimani na Chamanangwe. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 10.80 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ujenzi wa Kituo cha Maonesho Chamanangwe - Pemba; na
ii. Ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa, jengo la kuuzia chakula, eneo la kufurahishia watoto pamoja na ukumbi wa mikutano wa kisasa katika kituo cha Dimani.

***Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Parks)***

Mradi huu una lengo la kukuza uchumi kupitia uimarishaji wa sekta ya viwanda na mazingira mazuri ya biashara katika maeneo makuu matatu Dunga, Pangatupu na Chamanangwe. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.56 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ujenzi wa majengo ya viwanda, utawala na sehemu ya kupokelea na kupakia mizigo katika eneo la Dunga na Chamanangwe;
ii. Ujenzi wa ukuta na vituo vya kusafisha maji machafu na kemikali katika eneo la Dunga na Chamanangwe;

iii. Ujenzi wa miundombinu ya umeme katika eneo la Dunga, Pangatupu na Chamanangwe;
iv. Ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara katika eneo la Chamanangwe na Pangatupu; na
v. Usimamizi wa shughuli za mradi.

### 7.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Sekta ya elimu ni msingi wa mafanikio ya kiuchumi na kijamii. Uwekezaji katika Sekta ya elimu ni muhimu katika mustakabali wa maendeleo ya Taifa, kwani huandaa kizazi chenye uwezo wa kutatua changamoto za sasa na zijazo kwa ufanisi. Ili kufikia mafanikio hayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwekeza zaidi Sekta hii kwa kuimarisha miundombinu pamoja na kupeleka vifaa vyenye viwango vya kujifunza na kufundishia. Kwa mwaka 2025/2026, Sekta ya Elimu imepanga kutekeleza Programu moja na Miradi miwili ya Maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 522.47 bilioni (TZS 321.86 bilioni kutoka Serikalini na TZS 200.62 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha Miundombinu ya Sekta ya Elimu kiujumla ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora yenye viwango na ufanisi. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 439.32 bilioni (TZS 247.65 bilioni kutoka Serikalini na TZS 191.68 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa skuli 20 za maandalizi, 17 za msingi (tisa za chini na nane za ghorofa) na 12 za ghorofa za sekondari;
ii. Kusaidia ujenzi wa skuli 21 (13 msingi na nane sekondari);
iii. Ukarabati wa madarasa 900 katika skuli mbali mbali;
iv. Ukamilishaji wa madarasa 300 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;
v. Ujenzi wa skuli tatu za Elimu Mjumuisho;
vi. Ujenzi wa vyoo 500 kwa skuli za maandalizi, msingi na sekondari;
vii. Kuziwekea miundombinu ya umeme wa jua skuli 19 za ghorofa za msingi;
viii. Ujenzi wa Karakana 25 kwa skuli za sekondari;

ix. Ujenzi wa dakhalia tisa na nyumba 10 za walimu;
x. Kuendelea na ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 ya wanawake na kuanza ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 wanaume katika chuo cha SUZA;
xi. Ujenzi wa Chuo cha Ubaharia;
xii. Ujenzi wa karakana za Uhandisi Mitambo, Uhandisi ujenzi, magari katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na kuzipatia vifaa
xiii. Kusaidia ujenzi wa ukumbi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Tekonolojia;
xiv. Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha IIT Madras;
xv. Kuvifanyia ukarabati vituo vya Ualimu (TCs), vituo vya Elimu Mbadala na Watu Wazima Rahaleo na Forodhani;
xvi. Kuendelea na ujenzi wa vyuo vitano vya Amali na Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
xvii. Kuanzisha Kituo cha kuchapisha mitihani na kukarabati Baraza la Mitihani;
xviii. Ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Habari za Elimu Kwarara - Unguja na Mkoroshoni - Pemba;
xix. Ukarabati wa Maabara za Kompyuta;
xx. Kujenga Maktaba Kuu ya kisasa; na
xxi. Kujenga viwanja viwili vya kisasa katika skuli zenye michepuo ya michezo na Ujenzi wa "Sports Academy".

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ujenzi wa skuli 20 za ghorofa (nane za msingi na 12 sekondari) Unguja na Pemba;
ii. Ukarabati wa madarasa 900 katika skuli za maandalizi, msingi na sekondari;
iii. Ukamilishaji wa madarasa 300 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi;
iv. Ujenzi wa vyoo 200 katika skuli za maandalizi, msingi na sekondari;
v. Kuendelea na ujenzi wa skuli 3 zenye dakhalia;
vi. Ujenzi wa jengo la utawala, skuli ya elimu, nyumba za wafanyakazi, kituo cha wanafunzi na kiwanja cha michezo katika chuo cha SUZA;
vii. Ujenzi wa Chuo cha Ubaharia Beitras;
viii. Kuunganisha mkonga wa Taifa na skuli, vituo vya ubunifu wa kisayansi (HUBs) na vituo vya ualimu (TCs);

ix. Ujenzi wa karakana za uhandisi mitambo, uhandisi ujenzi, magari na kuzipatia vifaa katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume;
x. Ujenzi wa jengo la skuli ya kilimo na maabara ya sayansi ya kisasa na utoaji wa taaluma ya mahitaji maalum katika Kampasi ya Tunguu;
xi. Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Amali kwa kila Mkoa; na
xii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara Chake Chake- Pemba.

***Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote kwa kuwapatia walimu na wanafunzi vifaa vya kujifunzia na kufundishia, mafunzo ya malimu na matumizi ya TEHAMA. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 48.15 bilioni (TZS 39.21 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali.***

i. Ununuzi wa vifaa vya usafi, maabara na maktaba kwa ajili ya skuli mpya;
ii. Kuimarisha miundombinu ya skuli/dakhalia kwa kuziwekea mifumo ya gesi asilia;
iii. Kuziwekea miundombinu ya umeme wa jua skuli 15 za ghorofa za sekondari;
iv. Ununuzi wa magodoro 10,000 kwa ajili ya dakhalia mpya;
v. Kuzipatia Karakana vifaa vya kufanyia mazoezi;
vi. Kuwapatia walimu mafunzo ya fani ya Amali na Ufundi ;
vii. Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vitabu kwa ajili ya Mtaala mpya;
viii. Kuzipatia skuli vifaa vya michezo na vifaa vya TEHAMA zikiwemo "Smart Screen", "Desktop", "Laptop" na "Printer"; na
ix. Ununuzi wa samani kwa ajili ya skuli za maandalizi, msingi na sekondari.

***Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya Maktaba Kuu na Maktaba za Wilaya;
ii. Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vitabu kwa ajili ya Mtaala mpya;
iii. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Maktaba Mtandao katika skuli 33 za Unguja na Pemba na kuwapatia mafunzo maafisa 10 wa Wizara, wakufunzi 50 na walimu 1,200; na
iv. Kusaidia mafunzo ya lugha ya Kiarabu.

***Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu***

Lengo la mradi huu ni kuongeza idadi ya wataalamu wazalendo katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa kutekelezwa***

- Kuwapatia mikopo wanafunzi wa Elimu ya juu Zanzibar.

### 7.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Wizara hii inatekeleza majukumu yake ya utoaji wa habari kwa wasikilizaji na watazamaji kupitia magazeti, TV na Redio, kuwawezesha vijana kwa kuwatafutia fursa za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza Programu moja na miradi miwili ya Maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 433.58 bilioni (TZS 432.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Kuendeleza Viwanja ya Michezo**

Programu ina lengo la kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kiasi cha TZS 414.08 bilioni (TZS 413.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa kiwanja kipya cha mpira pamoja na viwanja viwili vya mazoezi;
ii. Ujenzi wa Hospitali na hoteli ya kisasa (4 star); na
iii. Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya na Mkoa.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

- Ujenzi wa viwanja sita vyenye miundombinu ya michezo ya aina nne katika kiwanja kimoja (four in one) Unguja na Pemba.

***Mradi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili***

Mradi una lengo la kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha na ufundi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa vituo vya mafunzo ya vijana Awamu ya II Pangeni - Unguja na Ole - Pemba;
ii. Ununuzi wa vifaa na samani vya kituo cha mafunzo kwa vijana Bweleo Unguja na Weni - Pemba;
iii. Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mabaraza ya vijana na vikundi vya kiuchumi Unguja na Pemba; na
iv. Ujenzi wa kituo cha maendeleo ya vijana Muyuni - Unguja.

***Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni***

Lengo la mradi ni kuweka miundombinu kwa ajili ya mafunzo na utaalamu wa sanaa katika tasnia ya sanaa ikiwemo kuibua, kukuza na kuhuisha vipaji kwa vijana ili kukuza ajira na vipato vyao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe; na
ii. Ununuzi wa samani na vifaa vya Ofisi.

### 7.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara imehusisha sekta muhimu katika ukuzaji uchumi kwa kutoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kupambana na umasikini, kuongeza uzalishaji, kuwa na uhakika wa chakula, utoaji wa ajira pamoja na kuimarisha huduma. Wizara pia inasaidia upatikanaji wa pembejeo na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu na miradi minne itakayogharimu jumla ya TZS 58.18 bilioni (TZS 24.70 bilioni kutoka Serikalini na 33.48 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

Programu imeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga, kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa uzalishaji kwa kutumia pembejeo za kilimo. Kwa mwaka 2025/2026, programu inatarajia kutumia TZS 5.81 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha malipo kwa kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la Cheju 'B';
ii. Kukamilisha ununuzi wa mitambo midogo ya kusaidia kazi za kilimo ikiwemo kupalilia na uvunaji katika mabonde ya umwagiliaji; na
iii. Kusimamia maeneo yaliyojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji.

**Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo**

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu inatarajia kutekeleza miradi minne (4) kama ifutavyo:-

***Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii za wafugaji na wakulima, kuimarisha miundombinu ya utafiti wa mifugo na kudhibiti ndege waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru) pamoja na kuimarisha maudhui ya kilimo TV. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrojeni ili kuhifadhia mbegu za madume kwa ajili ya kupandishia ng'ombe kwa njia ya sindano;
ii. Ujenzi wa miundombinu ya karantini ya Kisakasaka–Unguja na Gando Nziwengi – Pemba;
iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugo ikiwemo maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama, mabanda ya mbuzi, kuku, kondoo na Ofisi Unguja na Pemba;
iv. Kudhibiti wanyama waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru); na
v. Kuzindua na kuimarisha maudhui ya kilimo TV.

***Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki***

Mradi huu una lengo la kuimarisha sekta ya ufugaji nyuki isaidie katika ukuaji wa uchumi shirikishi pamoja na kuiwezesha asali inayozalishwa kuwa na viwango vya ubora na kukubalika katika masoko ya ndani na nje. Mradi huu unatekelezwa kisiwani Pemba na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa jumla ya TZS 100.0 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha na kuendeleza hifadhi za nyuki katika misitu ya jamii;
ii. Kuendeleza upatikanaji wa pembejeo za ufugaji nyuki; na
iii. Kutoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki.

***Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unazingatia Mabadiliko ya Tabianchi.***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuchangia katika kuleta mageuzi kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya kukuza hali ya maisha kwa jamii. Mradi unatarajiwa kuongeza uhakika wa chakula pamoja na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Mradi pia utasaidia kukuza kipato, uhimilivu wa tabianchi na kuongeza lishe kwa wazalishaji wadogo wadogo wa maziwa. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.25 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukarabati wa vituo vya Jumuiya za ukusanyaji na usarifu maziwa;
ii. Ujenzi wa vituo vipya na viwanda vidogo vidogo vya ukusanyaji na usarifu maziwa katika maeneo maalum;
iii. Ununuzi wa mitamba bora ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa;
iv. Ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu yaliyopo Kizimbani;
v. Kufundisha maofisa ugani njia bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia bora za kisasa;
vi. Kufundisha wafugaji njia bora za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuzingatia namna za uhimilivu wa tabianchi; na
vii. Ununuzi wa mitambo ya 'biogas plant' kwa lengo la upatikanaji wa nishati ya kupikia na mbolea kwa ajili ya uzalishaji wa mazao pamoja na malisho ya mifugo Unguja na Pemba.

***Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuchangia uimarishaji na uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato kwa wakulima wa mpunga Zanzibar pamoja na kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka

2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 3.95 bilioni (TZS 200.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.75 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ununuzi wa matrekta ya kilimo katika mabonde ya umwagiliaji, ununuzi wa mashine ya kuvunia mpunga na kutoa mafunzo kwa Jumuiya za wakulima wa mpunga;
ii. Kuboresha miundombinu ya kilimo kwa kutengeneza njia za mashambani, vivukio vya matrekta pamoja na maeneo ya kuanikia mpunga;
iii. Kujenga maeneo ya kuhifadhia matrekta, mazao ya mpunga pamoja na uchimbaji wa kisima katika kuongeza upatikanaji wa maji katika bonde la Chaani; na
iv. Ununuzi wa vifaa vya usimamizi na ufuatiliaji wa vyanzo vya maji katika maeneo ya umwagiliaji.

**Programu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Chakula**

Programu ina lengo la kusimamia sekta za kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa mazao ya kilimo yaliyosalama, upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kitaifa pamoja na kuwajengea uwezo wakulima juu ya mifumo ya chakula. Kwa mwaka 2025/2026, programu inatarajia kutekeleza miradi mitano ya Maaendeleo:-

*Mradi wa ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula*

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwa na upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa kwa ukarabati wa maghala ya chakula na ujenzi wa vihenge. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.00 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ukarabati wa maghala tisa (Unguja matatu na Pemba sita) pamoja na ununuzi wa chakula; na
ii. Ununuzi wa mitambo ya baridi katika maghala.

*Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania*

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu

katika mifumo ya chakula. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 12.50 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza hatua za ukarabati wa majengo ya maabara, miundombinu ya mbegu na vituo vya huduma kwa wakulima;
ii. Kutoa mafunzo kwa maofisa ugani juu ya namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari na mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia ya kilimo shadidi na kuwafundisha vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo;
iii. Kuendeleza tafiti ili kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; na
iv. Kukamilisha usarifu wa michoro kwa mabonde 16, kutafuta wajenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi.

***Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi***

Mradi una lengo la kuhifadhi misitu katika maeneo ya Kaskazini 'A' na 'B', kushirikisha sekta za kilimo, mazingira, ardhi na sekta nyengine zenye mnasaba pamoja na uhifadhi wa misitu na kusimamia rasilimali hiyo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.20 bilioni.

**Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa**

i. Kukarabati majengo ya vituo vya wakulima Kaskazini - Unguja;
ii. Kuhamasisha utunzaji wa mazingira, kupanda miti, uoto wa kuzuia uharibifu wa mazingira kwa jamii zinazozunguka Wilaya za Kaskazini 'A' na 'B'; na
iii. Kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu.

***Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi***

Mradi una lengo la kubadili mifumo ya chakula ili kuchochea uchumi jumuishi, kuongeza usalama wa chakula na lishe nchini pamoja na kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya chakula ikiwemo: migomba, mihogo na mwani kwa kutumia mbinu jumuishi zinazokabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuongeza

ujuzi na uwezo wa vijana na wanawake waweze kujiajiri na kupata fursa za kilimo katika miradi ya kijamii. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.44 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa vifaa vya umwagiliaji na uzalishaji wa mazao ya baharini;
ii. Kuanzisha mashamba ya mfano ya uzalishaji kibiashara kwa kutumia dhana ya shamba darasa;
iii. Kuanzisha mashamba ya kibiashara ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mihogo;
iv. Kutoa taaluma ya uhifadhi wa mazao, uongezaji wa thamani, ubora wa bidhaa na utafutaji wa masoko; na
v. Kutengeneza Mpango Mkakati wa zao la mwani na kushauri muundo wa kitaasisi.

***Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha Usalama wa Chakula***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mfumo wa Kitaifa wa udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo, kuongeza upatikanaji mazao ya kilimo na kukuza masoko ya Kitaifa na Kimataifa. Vile vile, kuimarisha afya ya mimea na mifumo ya ulinzi wa mimea. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.37 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ukamilishaji wa rasimu ya Kanuni za afya ya mimea Zanzibar;
ii. Kukamilisha ujenzi wa maabara kuu za afya ya mimea katika ofisi za Kitengo cha Utibabu na Ukaguzi wa Mazao, Unguja na Pemba;
iii. Kukamilisha ujenzi wa maabara ndogo katika afisi za Kitengo cha Utibabu wa Mimea na Ukaguzi wa Mazao Bandarini – Malindi;
iv. Kukamilisha ujenzi wa maabara ndogo za kontena katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, bandari ya Mkoani na Wete Pemba;
v. Kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha Utibabu wa Mimea na Ukaguzi wa Mazao;

vi. Kuimarisha matumizi ya mfumo wa utoaji vibali vya afya ya mimea wa e – kilimo;
vii. Kuanzisha mkakati wa udhibiti wa maradhi ya migomba hususani "Banana Bunch Top Virus" (BBTV);
viii. Kuwajengea uwezo marubani wa 'drone' juu ya kufanya upembuzi wa taarifa (analysis of multispectral data); na
ix. Kukamilisha manunuzi ya gari na pikipiki kwa ajili ya kufuatilia shughuli za afya ya mimea.

***Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufuma -Pongwe***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwaunganisha na kuwalinda wanyama adimu ambao wanapatikana katika hifadhi, kuongeza mapato yatokanayo na rasilimali za Misitu kwa Shehia zitakazonufaika na mradi. Kupitia Mradi huu zimetangazwa rasmi hekta 1,988 za msitu kuunganisha hifadhi za Jozani na Kiwengwa pamoja na kuimarisha usimamizi na kuongeza alama za vipimo vya ufuatiliaji na usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS120.00 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa ramani za eneo lililopendekezwa na kuutambulisha mradi kwa wadau;
ii. Kufanya Mapitio ya Mkataba wa Usimamizi wa Misitu ya Jamii na kuzitangaza katika gazeti rasmi la Serikali;
iii. Kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi shirikishi kwa jamii ikiwemo wanafunzi;
iv. Kufanya mapitio ya azma na kuitangaza hifadhi (Final order); na
v. Kuandaa mfumo wa kuweka kumbukumbu ya malalamiko na kero za wanajamii.

***Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Mimea (Botanic Garden)***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuinua mapato ya Serikali kupitia ada ya wageni wanaotembelea shamba la viungo na bustani ya mimea, kusaidia kuimarisha shamba lenye aina nyingi za mimea na kuweka mandhari ya kuvutia wageni wengi zaidi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya ubunifu wa bustani ya mimea;
ii. Kuchimba kisima na kuweka miundombinu ya umwagiliaji maji;
iii. Kuanzisha shamba ndogo ndogo za miti ya viungo na madawa;
iv. Kurudisha uoto wa asili na miti adimu na iliyo hatarini kutoweka;
v. Kuwajengea uwezo wataalamu kuhusu taaluma ya kutoa huduma za mimea ya viungo na madawa kwa wageni;
vi. Ujenzi wa jengo la mapokezi na Ofisi ya kutoa huduma za utalii wa viungo (spice tourism);
vii. Kuboresha njia za ndani ya shamba, kuweka mabango, nembo, geti na maegesho ya magari;
viii. Kuanzisha tovuti na kuchapicha vipeperushi kwa ajili ya kulitangaza shamba la viungo na bustani; na
ix. Kuweka ulinzi kupitia vikosi vya SMZ.

***Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo***

Mradi una lengo la kuwajengea uwezo mabibi na mabwana shamba ili wawe na ubunifu na uwezo zaidi wa kuwaelimisha wakulima kwa kutumia mbinu/ njia bora za uzalishaji wa mazao kwa kutumia pembejeo zilizopo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 400.00 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya sensa ya wakulima, aina ya mazao na maeneo wanayolima;
ii. Kuanzisha ‘Demo plot’ 446 zenye ukubwa tofauti;
iii. Kutoa mafunzo maalum kwa wataalamu na wakulima viongozi kuhusiana na uzalishaji wa mazao;
iv. Kuandaa mazingira ya upatikanaji wa pembejeo rahisi za kilimo; na
v. Kuanza na ujenzi wa kituo cha kutoa taarifa ‘Digital platform’ kwa kufanya maandalizi na upatikanaji wa vifaa stahiki kwa ajili ya kituo.

***Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakabali wa Sekta ya Kilimo***

Mradi huu una lengo la kuinua kipato cha vijana kupitia kilimo na biashara ya mazao ya mboga mboga. Mradi utasaidia vijana 98,000 hususan wanawake na wale walio kwenye hali ngumu kupata ajira za kuheshimika na zinazoridhisha

katika tasnia ya 'horticulture' Tanzania. Mradi utaongeza uzalishaji, ustahimilivu na uendelevu wa biashara za kilimo zinazomilikiwa na vijana. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 549.05 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandikisha vijana 98,000 watakaonufaika na mradi ambapo asilimia 70 wakiwa wanawake;
ii. Kuteua na kufunza vijana, hususan wanawake kama wakulima viongozi (village-based advisors);
iii. Kuhamasisha ushiriki wa vijana kwenye miradi maalum ya Serikali;
iv. Kufundisha vijana mbinu bora za kilimo, ikiwemo kilimo cha mboga mboga na uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna;
v. Kuwafundisha vijana kilimo biashara; na
vi. Kuunganisha vijana na masoko.

## 7.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii kwa upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto sambamba na kushajihisha maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 6.49 bilioni (TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.99 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Hifadhi ya Wazee***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kukuza ustawi wa wazee kwa kuimarisha usalama wao, kuhakikisha wanaishi katika makaazi mazuri na wanapata huduma zao za msingi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukarabati wa makaazi ya wazee Limbani na Sebleni; na
ii. Ununuzi wa vifaa na samani.

***Mradi wa Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana***

Mradi una lengo la kuimarisha haki za wanawake na wasichana kwa kupambana na ukatili wa kijinsia sambamba na uhamasishaji na haki za binaadamu. Kwa

mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 636.32 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya tathmini ya vituo vya mkono kwa mkono Unguja na Pemba;
ii. Kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na ukatili na udhalilishaji; na
iii. Kuhamasisha wanawake kujua haki na wajibu wao.

***Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)***

Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji Tanzania. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 4.35 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu;
ii. Kupinga na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji; na
iii. Usimamizi na uratibu wa mradi.

### 7.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara hii inasimamia sekta kuu tatu ambazo ni maji, nishati na madini ambazo ni nguzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi pamoja na ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutumia jumla ya TZS 205.36 bilioni (TZS 65.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 139.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza Programu mbili:-

**Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutekeleza miradi tisa ya maendeleo:-

***Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar***

Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar (Miji 25 - INDIA) ni sehemu ya juhudi upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira Zanzibar. Kazi kuu za mradi ni uimarishaji wa huduma za Maji Endelevu Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 16.17 bilioni (TZS 2.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.65 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Ziliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Uendeshaji wa shughuli zilizoanzishwa na mradi; na
ii. Malipo ya utangulizi kwa Mshauri Elekezi na Wakandarasi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Malipo ya awali ya Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi; na
ii. Malipo ya Mshauri Elekezi na Mkandarasi kwa ajili ya kazi za usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya maji.

***Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar***

Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji kwa kufanya usambazaji na uzalishaji wa maji safi na salama katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 15.78 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji na uhifadhi wa maji Unguja na Pemba;
ii. Uwekaji wa uzio katika maeneo ya hifadhi ya maji; na
iii. Ununuzi wa pampu maalumu, vifaa na bomba za kusafirishia maji.

***Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Mkoa wa Mjini Magharibi***

Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji na usambazaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya zake ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 41.49 bilioni (TZS 1.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 39.95 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

- Ulipaji wa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na mradi.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa Kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

i. Malipo ya Mshauri Elekezi na Wakandarasi; na
ii. Ununuzi wa vifaa.

*Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali Maji Chini ya Ardhi*

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamiaji wa rasilimali maji pamoja na uimarishaji wa huduma za uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.68 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Malipo ya Mshauri Elekezi;
ii. Uendeshaji wa mradi; na
iii. Kujenga uwezo kwa watendaji.

*Mradi wa Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja*

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji hususan katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kufanya ukarabati wa visima na kuweka miundombinu ya umeme na pampu zinazotumia umeme wa jua kwa ajili ya kuendeshea visima hivyo. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya National Energy Centre (NEC) ya Oman. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kukarabati na kuchimba visima vipya pamoja na ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji; na
ii. Kuweka mifumo ya umeme wa jua katika visima na kununua pampu zinazotumia umeme huo.

*Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar*

Mradi huu una lengo la kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya kisiwa cha Pemba. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya

Ujerumani (KfW). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 71.43 bilioni (TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 68.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Uendeshaji na usimamizi wa mradi.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa matangi; na
ii. Malipo kwa ajili ya Mshauri Elekezi na Wakandarasi wa mradi.

***Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi Katika Maeneo ya Mijini***

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamizi wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Mradi umelenga kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kusaidia Wizara katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabinchi na uchafuzi wa kimazingira na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara. Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa miongozo mbali mbali ya sekta ya maji na usafi wa mazingira;
ii. Kuwajengea uwezo watendaji kutoka Wizarani, ZURA, ZAWA pamoja na Serikali za Mitaa;
iii. Kusimamia na kuwezesha upatikanaji wa taarifa za rasilimali maji; na
iv. Kusimamia upatikanaji wa matumizi bora ya rasilimali maji.

***Mradi wa Kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za maji safi na usafi wa mazingira Zanzibar na miundombinu ya maji, kuongeza upatikanaji wa maji safi, na kuimarisha usafi wa mazingira kwa kutumia teknolojia za kisasa na ushirikiano wa kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.36 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Malipo kwa ajili ya Mshauri Elekezi wa uandaaji wa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira.

***Mradi wa Ununuzi wa "Chlorine", Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji***

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa jamii, unahusisha pia ununuzi wa "chlorine" kwa ajili ya kutibu maji, kuhakikisha usimamizi bora wa rasilimali za maji na ufuatiliaji ubora wa maji ili kupunguza magonjwa yanayohusiana na maji yasiyo salama. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 40.00 milioni kutoka Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa za kutibia maji (chlorine).

**Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar**

Programu ina lengo la kuwa na umeme wa kujitosheleza ikiwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha shughuli za kiuchumi, usafiri na huduma za jamii. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepanga kutekeleza miradi minne ya maendeleo:-

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za umeme pamoja na miundombinu ya umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kupata huduma ya umeme yenye uhakika. Kukamilika kwa mradi huu kutapunguza changamoto ya upungufu wa umeme katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.00 bilioni kutoka Serikalini.
Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Usambazi wa umeme katika vijiji vya Unguja na Pemba;
ii. Ununuzi wa nguzo na vifaa vya umeme; na
iii. Uvutaji wa njia mpya za umeme.

***Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA)***

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.47 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuendelea na ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi;
ii. Uwekaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya umeme;
iii. Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua pamoja vituo vya kupozea umeme katika maeneo ya Makunduchi, Ubago na Matemwe;
iv. Kusimamia masuala ya jinsia katika sekta ya nishati; na
v. Kuwajengea uwezo watendaji katika sekta ya nishati.

*Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar*

Mradi huu unalengo la kuboresha Mfumo wa Umeme Zanzibar na kuondoa changamoto ya umeme mdogo pamoja na kukatika kwa umeme mara kwa mara. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 33.36 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umeme na kuweka vifaa maalumu vya kudhibiti na kuongeza nguvu za umeme; na
ii. Kufanya Malipo kwa ajili ya "Distribution Management System - Phase 1" Awamu ya kwanza.

*Mradi wa Ulazaji wa Waya wa umeme Bahari*

Mradi huu una lengo kuondoa changamaoto za umeme kwa ujenzi wa miundombinu ya nyaya za chini ya bahari kwa Unguja na Pemba. Mradi huu unalenga kuweka waya mpya wa Megawati 200/220KV kwa Unguja, Megawati 100/132KV kwa Pemba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupokelea umeme katika maeneo ya Kusini Unguja na Mkumbuu kwa Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 3.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa*

- Kukamilisha taratibu za manunuzi za kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa utengenezaji wa nyaya za baharini, vifaa na usafirishaji wa umeme chini ya bahari.

## 7.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Wizara hii ina lengo la kuigeuza Zanzibar kuwa kitovu cha maendeleo ya Uchumi wa Buluu sambamba na kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharí, kupitia fursa za uwekezaji katika uchumi wa buluu ikiwemo uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha bahari, ufugaji wa mazao baharini, utalii wa baharini na fukwe, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na uratibu wa utawala na mazingira ya baharini. Wizara imedhamiria kuwawezesha wajasiriamali katika kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya biashara na viwanda ambazo zitasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza Programu nne na mradi mmoja wa maendeleo ambayo imepangiwa jumla ya TZS 157.08 bilioni (TZS 131.24 bilioni kutoka Serikalini na TZS 25.84 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo)

**Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi**

Programu hii ina lengo la kuongeza faida katika biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki, kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kiasi cha TZ 13.14 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa meli ya uvuvi wa bahari kuu;
ii. Ununuzi wa gari aina ya lori na jokofu la tani 10 kwa ajili ya kampuni ya ZAFICO;
iii. Kuanzisha mashamba darasa mawili ya ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa na matangi na kuanzisha Karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo Unguja na Pemba;
iv. Kuendelea kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za mazao ya baharini (majongoo bahari, kaa na mwatiko);
v. Ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya uvuvi na ufugaji wa viumbe bahari Unguja na Pemba;
vi. Kuandaa mpango wa ushirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa kuendesha kiwanda na meli;
vii. Ujenzi wa vituo vya kusarifu mwani;
viii. Ununuzi wa mashine tano za kuchakata mwani na vifaa vya kuongeza thamani zao la mwani;

ix. Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wa mwani kwa kutumia njia ya za kisasa (double loop method); na
x. Kuwapatia vifaa vijana wanaojitolea wa kituo cha 'Building Better Tomorrow' kwa lengo la kuwasaidia kuongeza kipato chao.

**Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia**

Programu hii ina lengo la kuboresha miundombinu inayohusiana na uzalishaji, usambazaji na uhifadhi wa mafuta na gesi asilia, pamoja na kuweka mifumo ya usimamizi wa mafuta na gesi kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Zanzibar. Programu inajumuisha miradi miwili:-

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia***

Mradi una lengo la kuimarisha Usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia kupitia kituo cha Taifa cha kuhifadhi taarifa, ili kuhakikisha taarifa hizo zinatunzwa kwa usahihi na usalama. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 7.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza na ujenzi wa kituo cha kuhifadhi taarifa za mafuta na gesi Kisakasaka.

***Mradi wa Usambazaji wa Gesi***

Mradi una lengo la kuimarisha usalama wa nishati kwa kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi na salama kwa matumizi ya majumbani pamoja na kuhifadhi mazingira. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 9.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa kituo cha gesi iliyoshinikizwa kutoka Tanzania Petrolium Cooperation (TPDC) - Dar es Salaam;
ii. Ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi asilia kutoka Tanzania Petrolium Cooperation (TPDC) na kusambaza katika maeneo ya Zanzibar;
iii. Ununuzi wa vituo vitano vya gesi asilia iliyoshinikizwa vinavyohamishika (mobile station);
iv. Ununuzi wa magari na trela tano za kuchukulia gesi asilia iliyoshinikizwa; na
v. Ujenzi wa bomba la usambazaji gesi asilia (1.5 km).

**Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Mazao ya Baharini**

Programu ina lengo la kusimamia na kuimarisha mazao ya baharini ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. Programu inajumuisha miradi mitatu:-

***Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mwani***

Mradi una lengo la kuongeza uzalishaji wa zao la mwani kwa kuweka mazingira ya upatikanaji wa vifaa, huduma na masoko. Mradi utaimarisha uhusiano na wadau mbali mbali ili kuwawezesha wakulima wa mwani kwa kuwapatia mitaji, ujuzi, teknolojia na uwezo wa kiutawala ili kuongeza uzalishaji na mapato. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.58 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa viwanda vya mwani Unguja na Pemba;
ii. Kufanya utafiti wa upatikanaji wa masoko kwa bidhaa ya mwani;
iii. Kutengeneza mpango wa usimamizi wa mfuko wa makubaliano ya soko la mwani; na
iv. Kuandaa Mikataba yenye masharti nafuu na Mpango wa biashara kwa wakulima wa mwani.

***Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini***

Mradi una lengo la kuwawezesha wakulima wa mwani na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu kwa kuongeza mnyororo wa thamani. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.69 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha mashamba manne ya majaribio ya mwani na majongoo bahari;
ii. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani Chokocho- Pemba;
iii. Kutoa mafunzo kwa wanawake 2000 wakulima wa mwani na majongoo bahari;
iv. Utoaji wa vifaa kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini;
v. Ununuzi wa gari mbili za mradi Unguja na Pemba; na

vi. Kutoa mafunzo ya teknolojia ya kisasa ya kilimo cha mwani, kaa na majongoo bahari.

***Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania***

Mradi una lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa walengwa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 10.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa Ofisi ndogo sita katika maeneo ya hifadhi, Tumbatu, Mnemba, Huba Chwaka, Huba Menai na Mkondo wa Pemba;
ii. Ununuzi wa boti saba za doria;
iii. Kufanya ukarabati wa jengo la Nyangumi- Unguja na Jodari – Pemba;
iv. Ununuzi wa vifaa na boti mbili za Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Tanzania bara na Zanzibar; na
v. Ujenzi wa madiko na masoko mawili ya samaki Kizimkazi na Chwaka.

**Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Uvuvi**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya sekta ya uvuvi ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi, kukuza ajira, kuongeza kipato cha wavuvi na kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa. Programu inajumuisha miradi mitatu:-

***Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi***

Mradi huu una lengo la kuimarisha mazingira ya wavuvi kwa kujenga miundombinu itakayochochea ukuaji wa Sekta ya uvuvi. Mradi umepangiwa kiasi cha TZS 29.99 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza kwa ujenzi wa bandari ya uvuvi Shumba - Pemba.

***Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki***

Mradi una lengo la kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea miundombinu ya kisasa ya kuhifadhia na kuuzia samaki katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 27.68 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa madiko na masoko katika maeneo ya Kama, Bumbwini, Nungwi na Kizimkazi kwa Unguja na kwa Pemba Kiwani, Kengeja na Msuka.

***Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki***

Mradi huu una lengo la kuimarisha mnyororo wa sekta ya uvuvi na uongezaji wa thamani wa bidhaa ya dagaa kupitia usindikaji wa kisasa pamoja na kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa dagaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka wa 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 51.00 bilioni kutoka Serikalini

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Fungurefu, Ndagoni na Kama.

***Mradi wa Utafiti wa Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii***

Mradi una lengo la kupendekeza mikakati ya kukuza uchumi wa jamii, kuimarisha usalama wa chakula na maisha mazuri kwa jamii kwa kutumia mbinu shirikishi na endelevu za utafiti na maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 13.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kutoa udhamini wa masomo kwa elimu ya juu ili kudumisha uchumi, usalama wa chakula na maendeleo endelevu kwa jamii.

## 7.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara ina lengo la kuimarisha miundombinu wezeshi itakayochochea ukuaji wa Uchumi. Wizara inatekeleza miradi kupitia sekta kuu tatu ambazo ni Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Wizara imepanga kutekeleza programu tano na miradi miwili ya maendeleo kwa jumla ya TZS 1,549.46 bilioni (TZS 923.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 625.51 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara**

Programu inalengo la kuendeleza sekta ya miundombinu na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi nchini, kwa kuweka miundombinu itakayounganisha miji na maeneo mengine ya kiuchumi. Programu itaendeleza ujenzi na matengenezo ya barabara kuu pamoja na barabara za kuunganisha maeneo yenye kutoa huduma

za kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii itatekeleza miradi minne:-

***Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu***

Mradi una lengo la kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari ili kuhuisha uchumi na uwekezaji. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 329.03 bilioni (TZS 133.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 195.64 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Usafishaji wa maeneo ya barabara;
ii. Kuendeleza ujenzi wa misingi ya maji ya mvua, uwekaji wa michoro, alama na taa za barabarani;
iii. Kuendelea na ujenzi wa kilomita 277 za barabara kuu Unguja na Pemba;
iv. Usimamizi wa ujenzi wa barabara ya Tunguu – Makunduchi (48km) Mkoani – Chake Chake (km 43.5) na Fumba – Kisauni (12km) kwa kiwango cha lami;
v. Kuanza ujenzi wa barabara ya Amani – Dunga - Chwaka (km 27.42) kwa kiwango cha lami;
vi. Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tazari - Kilimani (km 3.5), Mkokotoni bandarini (km 1.4), Bumbwini-Pangatupu-Mahonda (km11.3) na daraja la Pangatupu, Mahonda-Zingwezingwe-Mangapwani (km 8.4), Mfenesini-Mangapwani (km 7.2); na
vii. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Wete - Chake Chake (km 8).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuanza ujenzi wa barabara ya Mkoani – Chake Chake (km 43.5), Tunguu – Makunduchi (48km) na Fumba – Kisauni (12km) kwa kiwango cha lami; na
ii. Kukamilisha ujenzi kwa barabara ya Wete - Chake Chake (km 8).

***Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani***

Mradi utahusisha ukarabati wa barabara za ndani na vijijini zenye urefu wa kilomita 275.9 km za awali na kilomita 65 mpya katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Mradi utaunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara kuu itakayosaidia kupunguza msongamano katika barabara

kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha miji na mitaa katika maeneo ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 78.03 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa barabara (km 34) ikiwemo Kitope - Ndagaa– Kidimni (km 19), Ndagaa - Mwakaje (8km) na Kibuteni - Kizimkazi (km 7);
ii. Uwekaji wa taa za barabarani katika maeneo ya Mangapwani-Mfenesini na eneo la hospitali ya Wilaya ya Kaskazini "B";
iii. Ujenzi wa barabara ya Kianga - Jitimai (km 3), Langoni-Kisauni kwa bi Asha (4.5km), Ubago-Jumbi (km 6.5), Mbuzini-Kijichi (km 6), Gando-Wete-Konde (km 26.5), Mtambile-Kengeja (10km), Goli la Mpira-Kwapopo (km 4.2), Mihogoni-Uhanga-Amani (km 2.2), Skuli ya Pujini-Chuo cha Mwalimu Nyerere (km 2.6);
iv. Ujenzi wa barabara za Tumbatu, Kazole-Matetema-Zingwezingwe (km5.3), Fuoni-Kipungani (km 9.2), Skuli ya Fuoni na Hospitali ya Tawakal (km 1);
v. Ujenzi wa barabara ya Regezamwendo (Mwera)-Kianga-Mfenesini (km 14.3); na
vi. Ujenzi wa barabara zinazounganisha mahoteli na barabara kuu kwa upande wa Unguja (km 20).

***Mradi wa Matengenezo ya Barabara za Mjini***

Mradi unalenga kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Kukamilika kwa mradi huu utaongeza haiba na kupendezesha Mji wa Zanzibar na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Usafishaji wa maeneo na kuanza uwekaji wa fusi na tabaka la lami kwa baadhi ya barabara;
ii. Kuendelea na ujenzi wa mitaro kwa baadhi ya barabara;
iii. Uwekaji wa taa na njia za waenda kwa miguu; na

iv. Kukamilisha ujenzi wa barabara za Mjini kilomita 20.9.

***Mradi wa Ujenzi wa Misingi ya Maji, Barabara pamoja na Matengenezo ya Maziwa Katika Maeneo ya Mji.***

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji machafu na ukusanyaji maji ya mvua katika mji wa Zanzibar ili kuweza kusaidia kupunguza mafuriko wakati wa mvua kubwa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 270.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i) Kujenga mitaro ya maji ya mvua;
ii) Kujenga mabwawa ya kutunzia maji ya mvua;
iii) Kujenga mifumo ya maji machafu; na
iv) Kujenga mitaro katika barabara zinazoendelea kujengwa.

**Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege**

Programu ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa vitakavyoweza kupokea ndege aina ya "code 4C", Programu itahusisha ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Pemba, Nungwi na "Terminal" II AAKIA. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 284.00 (TZS 124.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 159.50 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa Kwa Fedha za Serikali***

i. Kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria Terminal II AAKIA;
ii. Ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege katika uwanja wa AAKIA;
iii. Ujenzi wa Apron katika kiwanja cha ndege cha AAKIA;
iv. Ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi; na
v. Usimamizi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba;

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

- Ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

**Programu ya Kuimarisha Bandari**

Programu hii ina lengo la kujenga bandari jumuishi ya kisasa Mangapwani (Multipurpose Port) ambayo itajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta. Vile vile ujenzi wa chelezo cha kukarabati meli pamoja na bandari ya abiria na mizigo Maruhubi. Programu hii inatarajia

kutekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 335.10 bilioni (TZS 205.10 bilioni kutoka Serikalini na TZS 130.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa bandari ya makontena na mizigo mchanganyiko Mangapwani;
ii. Ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi pamoja na chelezo Mangapwani;
iii. Ujenzi wa jengo la Ofisi na ununuzi wa samani na vitendea kazi Mangapwani;
iv. Kukamilisha ujenzi wa nyumba 370 za fidia; na
v. Kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani (km 12) katika eneo la Mangapwani njia mbili.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuendeleza ufukiaji bahari (sea reclamation) katika eneo la Maruhubi;
ii. Kuendeleza ujenzi wa gati ya kupakia na kushushia mizigo (RoRo); na
iii. Ujenzi wa bandari ya abiria.

**Programu ya Mageuzi ya Kidigitali**

Programu hii ina lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao nchini. Programu itahusisha mifumo mbali mbali Serikalini inayotumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 76.05 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kulaza mkonga wa mawasiliano ya mtandao wa Kimataifa wa baharini (International Gateway) kutoka Mombasa-Kenya hadi Micheweni-Pemba kuelekea Fumba- Unguja;
ii. Utoaji wa huduma ya mtandao katika maeneo ya umma (Public Wi-Fi );
iii. Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center);
iv. Kufanya matengenezo na uwekaji wa mkonga;
v. Kutengeneza na kuunganisha mifumo ya mawasiliano ya TEHAMA; na
vi. Kukagua huduma za upatikanaji wa mawasiliano Zanzibar.

**Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG - Z)**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ambayo itashajihisha ukuaji wa uchumi katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 140.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa bwawa la Mwantenga na Ziwa Maboga;
ii. Ujenzi wa barabara ya Malawi na "Felix Momen" (km 3); na
iii. Ujenzi wa miundombinu ya barabara katika eneo la Michenzani (Michenzani Corridor).

***Mradi wa Uwekaji wa Kamera za Kusimamia Vyombo vya Usafiri Barabarani***

Mradi huu una lengo la kuimarisha usalama barabarani katika visiwa vya Zanzibar kwa kuweka kamera za kisasa ambazo zitakuwa na uwezo wa kutambua na kufuatilia mienendo ya vyombo vya moto pamoja na watumiaji wengine wa barabara. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.87 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukaguzi na kuandaa michoro kwa ajili ya uwekaji wa kamera za usalama barabarani;
ii. Uwekaji wa miundombinu na ufungaji wa kamera barabarani; na
iii. Kuunganisha mifumo ya kamera na mifumo mengine ya huduma za usafirishaji.

***Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar***

Mradi una lengo la kuimarisha upatikaji wa usafiri wa umma wa kisasa unaoendana na mabadiliko ya teknolojia na maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa TZS 374.34 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na Utafiti wa Mageuzi ya Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar.

## 7.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuongeza vivutio vipya vya utalii na kuendelea kuitangaza Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili na miradi miwili ya maendeleo inayotarajiwa kugharimu jumla ya TZS 37.03 bilioni (TZS 22.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.03 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria yaliopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Vile vile, Programu inasimamia kukuza shughuli za utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha makumbusho ya biashara na ununuzi wa samani eneo la Dunga;
ii. Kuanzisha makumbusho ya kisasa (Digital Museum) na ununuzi wa samani katika eneo la makumbusho ya viumbe hai Mnazimoja;
iii. Kuanzisha makumbusho ya Rais Abeid Amani Karume Mwera Zanzibar na ununuzi wa samani;
iv. Ujenzi wa uzio kwenye maeneo ya kihistoria ya Mwera, Pete, Dunga kwa upande wa Unguja, na Kuumbi, Mvuleni na Mwanampambe kwa Pemba; na
v. Ubunifu wa uundaji wa makumbusho ya Victoria Garden.

### Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii

Programu hii ina lengo la kuweka miundombinu ili kukuza na kuendeleza shughuli za utalii nchini, kwa kuendeleza, kuimarisha vivutio na kuongeza fursa za ajira pamoja na kukuza pato la Taifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuweka na kusambaza miundombinu ya maji na umeme katika mashamba ya utalii ya viungo Unguja na Pemba;

ii. Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na shughuli za utalii;
iii. Kuwaunganisha wazalishaji wa bidhaa za utalii pamoja na wanunuzi wakuu wa bidhaa hizo kwa lengo la kuinua masoko;
iv. Ujenzi wa majengo ya kutolea huduma "Service building" katika maeneo ya vivutio vya utalii Unguja na Pemba;
v. Kutoa elimu kwa watembezaji wa watalii juu ya historia ya Zanzibar na maeneo yake.

***Mradi wa Kulifanyia Ukarabati Jengo la Beit Al Jaib***

Mradi huu unalengo la kulinda na kurudisha jengo hilo ikiwa ni alama inayoitambulisha Zanzibar Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 15.03 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

Uendelezaji wa shughuli za kulifanyia matengenezo jengo la Beit Al Jaib.

***Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe***

Mradi huu una lengo la kulinda na kutunza majengo hatarishi yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe kwa kuyafanyia ukarabati. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS10.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ukarabati wa nyumba hatarishi zilizomo ndani ya eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe.

## 9.1 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kwa mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kusimamia na kufuatilia pamoja na kufanya Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Kufanya Tathmini ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo iliyokamilika na inayoendelea;
ii. Kujengea uwezo kwa Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali , Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia;
iii. Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050;

iv. Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini;
v. Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa Mpango wa Maendeleo wa muda wa kati 2026-2031;
vi. Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E Framework) wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026–2031;
vii. Kuandaa na Kuchapisha Ripoti ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa Zanzibar kwa mwaka 2025–2026; na
viii. Kuandaa nyenzo shirikishi za Ufuatiliaji wa Viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango Mpya wa Maendeleo wa Muda wa Kati wa Zanzibar 2026-2031 na Ajenda ya Afrika 2063.

## 10.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26, Washirika wa Maendeleo watakaochangia bajeti ya programu na miradi ya maendeleo ni pamoja na: ABUUDHABI-UAE, Adaptation Fund (AF), AfDB, ADF, AUSTRIA, BADEA, BENKI YA DUNIA, BIG WIN PHILANTHROPY, CHINA – EXIM BANK, EAC, ECDF - KOREA, ENABEL, EU, FAO, FCDO, GAVI, GERMAN/GIZ, GERMAN-KfW, GF, GIZ-KFW, HOWKLAND UNIVERSITY, IFAD, ILO, INDIA –EXIM BANK, IRISH EMBASSY, JICA, KFHI, KOICA, KOREAN GOVERNMENT, KUWAIT FUNDS, NETHERLAND, NORWAY, NORAD, OPEC, PHARM ACCESS INTERNATIONAL, SAUDI FUNDS, SIDA-GPE, SPAIN, STBF, SULTANATE OF OMAN, UAE, UKEF – CITI BANK, UKEF - DEUTCH BANK, UNCDF, UNDP, UNFPA, UNICEF, UNICREDIT BANK, UNIDO, UN-WOMEN, USAID, USAID-JHPIEGO, WB (IDA), WCS na WF.

## 11.0 HITIMISHO

Utayarishaji wa Kitabu cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo Mwaka 2025/2026 umeshirikisha wadau kutoka maeneo mbali mbali yakiwemo Wizara na Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na wananchi. Hivyo, kazi zilizoainishwa ndani ya Kitabu hiki zinatarajiwa kutekelezwa kwa matarajio ya kuweza kupata mafanikio ya kukuza uchumi ikiwa ni hatua ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050. Maeneo ya Vipaumbele vya Serikali yameainishwa, hivyo Wizara, Taasisi na Idara za Serikali wakitumie Kitabu hiki kwa madhumuni ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Programu na Miradi iliyoainishwa kupita katika sekta zao.

Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitaendelea na uratibu wa Mtiririko wa fedha (Cash Flow) za programu na miradi kuanzia mwezi wa Julai 2025. Hivyo, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zitaombwa kuwasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Programu/Mradi ya maendeleo. Inasisitizwa kuwa uwasilishaji wa maombi ya fedha uambatanishwe na vielelezo stahiki kwa mujibu wa shughuli za Programu/ Miradi kama Muongozo ya Serikali unavyoagiza.

Ili kuweza kupima na kujua ufikiaji wa matokeo yaliyokusudiwa, Wizara, Idara na Taasisi zinatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika Kitabu hiki wiki ya Pili ya kila robo mwaka (2025/2026) na kuziwasilisha Tume ya Mipango. Taarifa hizo zitajumuisha utekelezaji halisi na matumizi ya fedha, msisitizo ni kuwasilishwa kwa usahihi zenye usahihi zikiwemo za Serikali na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Sekta binafsi na Asasi za Kiraia zinaombwa ziwe na mikakati maalumu ya kuunga mkono juhudi za Serikali kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kurasa zifuatazo zina viambatisho ambavyo vinaonesha Mgawanyo wa fedha za Programu na Miradi ya Maendeleo Kiwizara kwa mwaka 2025/2026 kwa fedha za Serikali na za Washirika wa Maendeleo.

**PROGRAMU/MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025/2026**

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **A01** | **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Uimarishaji waMajengo ya Ikulu | 2,500,000 | 6,000,000 | | | | 6,000,000 |
| | ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mhe. Rais | 1,600,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | iii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano ya Mfumo wa Rais | 400,000 | 700,000 | | | | 700,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **8,700,000** | | **-** | **-** | **8,700,000** |
| **A09** | **TAASISI YA AFISI YA RAIS UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI** | | | | | | |
| | **Programu Shirikishi ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar** | | | BIG WIN PHILANTHROPHY | 1,323,000 | | 1,323,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **-** | **-** | | **1,323,000** | **-** | **1,323,000** |
| **A08** | **OFISI YA RAIS - UCHUMI NA UWEKEZAJI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji** | 15,000,000 | 15,000,000 | | | | 15,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **15,000,000** | **15,000,000** | **-** | **-** | **-** | **15,000,000** |
| **A011** | **WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa | 4,500,000 | 4,500,000 | UAE | 5,100,000 | | 9,600,000 |
| | ii) Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 32,000,000 | | | | | - |
| | iii) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | | | WORLD BANK | 1,000,000 | | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **36,500,000** | **4,500,000** | **-** | **6,100,000** | **-** | **10,600,000** |
| **F01** | **OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali | 80,261,187 | 59,576,410 | | | | 59,576,410 |
| | ii) Ujenzi wa Mji wa Serikali | 33,722,161 | 66,722,160 | | | | 66,722,160 |
| | **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | | BENKI YA DUNIA | | 32,500,000 | 32,500,000 |
| | **Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)** | 400,000 | 350,000 | NORWAY | | 4,400,000 | 4,750,000 |
| | **Programu ya Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo** | | 210,399,750 | | | | 210,399,750 |
| | **Mradi** | | | | | | |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | i) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili | 78,500 | 50,000 | | | | 50,000 |
| | ii) Msaada wa Kiufundi kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Uhamasishaji Utafutaji Rasilimali Fedha | | | WORLD BANK /UNCDF/BADEA/ GERMANY/GIZ | 276,150 | | 276,150 |
| | iii) Ulipaji wa Madeni kwa Miradi ya Maendeleo | 312,000,000 | 312,000,000 | | | | 312,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **426,461,848** | **649,098,320** | | **276,150** | **36,900,000** | **686,274,470** |
| **F03** | **TUME YA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar** | 3,000,000 | 4,500,000 | | | | 4,500,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo | | 5,500,000 | | | | 5,500,000 |
| | ii) Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa | 2,300,000 | 1,800,000 | | | | 1,800,000 |
| | iii) Kuendeleza Tafiti za Kimkakati | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,300,000** | **12,800,000** | | **-** | **-** | **12,800,000** |
| **F04** | **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | |
| | i) Mpango Mkuu wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) | | | WB | | 4,598,770 | 4,598,770 |
| | ii) Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia | | 2,000,000 | UN-WOMEN | 320,000 | | 2,320,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **-** | **2,000,000** | | **320,000** | **4,598,770** | **6,918,770** |
| **F05** | **OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | |
| | Mradi wa Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL) | | 1,023,875 | | | | 1,023,875 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | | **1,023,875** | | **-** | **-** | **1,023,875** |
| **G01** | **OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** | | | | | | |
| | **Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)** | 1,000,000 | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria** | 500,000 | 500,000 | UNDP/ IRISH EMBASSY | 1,229,877 | | 1,729,877 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Utoaji wa Huduma ya Haki kwa Kuzingatia Jamii | | | UN-WOMEN | 143,308 | | 143,308 |
| | ii) Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania (BSAAT) Programme | | | FCDO | 4,343,488 | | 4,343,488 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,500,000** | **1,500,000** | | **5,716,673** | **-** | **7,216,673** |
| **G02** | **MAHKAMA KUU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi *(ECMIS)* | 500,000 | | | | | - |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa | 24,900,000 | 13,000,000 | | | | 13,000,000 |
| | iii) Mradi wa Uboreshaji wa Mahkama | 600,000 | 600,000 | WORLD BANK | | 35,000,000 | 35,600,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **26,000,000** | **13,600,000** | | **-** | **35,000,000** | **48,600,000** |
| **D01** | **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | |
| | **Progamu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania** | | | BENKI YA DUNIA | | 2,100,000 | 2,100,000 |
| | **Miradi** | | | | | | - |
| | i) Kuimarisha Ulinzi na Usalama | 25,000,000 | 25,750,000 | | | | 25,750,000 |
| | ii) Kuimarisha Haki Jinai Chuo cha Mafunzo | 22,000,000 | 18,000,000 | | | | 18,000,000 |
| | iii) Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe | 29,000,000 | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | iv) Ujenzi wa Ofisi wa Masheha | 3,000,000 | 8,000,000 | | | | 8,000,000 |
| | v) Mradi wa Kijani na Kuimarisha Miji Sasa | | | EU | 8,271,970 | | 8,271,970 |
| | vi) Mradi wa Mji bila Taka | | 10,000,000 | | | | 10,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **79,000,000** | **81,750,000** | **-** | **8,271,970** | **2,100,000** | **92,121,970** |
| **D12** | **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 1,900,000 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | ii) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,900,000** | **3,500,000** | | **-** | **-** | **3,500,000** |
| **D04** | **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 2,650,000 | 2,500,000 | | | | 2,500,000 |
| | ii) Mradi wa Kuimarisha Shughuli za Uzamiaji na Uokozi | 2,460,040 | 2,500,000 | | | | 2,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,110,040** | **5,000,000** | | **-** | **-** | **5,000,000** |
| **D06** | **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ | 8,717,400 | 5,524,000 | | | | 5,524,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **8,717,400** | **5,524,000** | | **-** | **-** | **5,524,000** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **D03** | **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga - Chuo Cha Mafunzo | 2,550,000 | 3,578,000 | | | | 3,578,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,550,000** | **3,578,000** | | **-** | **-** | **3,578,000** |
| **D02** | **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi waNyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 1,640,000 | 5,986,000 | | | | 5,986,000 |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia | 1,500,000 | 3,125,100 | | | | 3,125,100 |
| | iii) Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU | | 5,423,000 | | | | 5,423,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,140,000** | **14,534,100** | | **-** | **-** | **14,534,100** |
| **D05** | **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari - KZU | 7,728,659 | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto | 2,500,000 | 2,550,000 | AUSTRIA | | 20,210,057 | 22,760,057 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **10,228,659** | **5,550,000** | | **-** | **20,210,057** | **25,760,057** |
| **B01** | **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | |
| | **Progamu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania** | | | BENKI YA DUNIA | 598,216 | | 598,216 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | 500,000 | 4,500,000 | | | | 4,500,000 |
| | ii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani | | | AF (UNDP) | 815,220 | | 815,220 |
| | iii) Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Kwanza wa Rais | 1,500,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,000,000** | **4,500,000** | **-** | **1,413,436** | **-** | **5,913,436** |
| **B04** | **MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA** | | | | | | |
| | **Progamu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania** | | | BENKI YA DUNIA | 152,100 | | 152,100 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | Mradi wa Kuirithisha Zanzibar Kijani | 1,500,000 | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,500,000** | **1,000,000** | | **152,100** | **-** | **1,152,100** |
| **C04** | **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA** | | | | | | |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya | 2,550,000 | 4,500,000 | | | | 4,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,550,000** | **4,500,000** | | - | - | **4,500,000** |
| **C01** | **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS - SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** | | | | | | |
| | **Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III)** | 100,000 | 100,000 | BENKI YA DUNIA | | 35,000,000 | 35,100,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Pili wa Rais | 4,500,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | ii) Ukarabati wa Ofisi ya Uratibu Dar es Salaam | 550,000 | 550,000 | | | | 550,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,150,000** | **2,650,000** | | - | **35,000,000** | **37,650,000** |
| **H01** | **WIZARA YA AFYA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | 645,000 | 1,000,000 | USAID/GF | 6,270,319 | | 7,270,319 |
| | **Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto** | 1,000,000 | 1,000,000 | GAVI/STBF/ UNFPA/ USAID-JHPIEGO | 5,281,065 | | 6,281,065 |
| | **Programu Shirikishi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | 380,000 | 1,000,000 | GF | 4,847,018 | | 5,847,018 |
| | **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya** | 27,500,000 | 35,350,000 | SULTANATE OF OMAN/ ABUUDHABI - UAE/Howkland University - NORWAY | 37,000,000 | | 72,350,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha huduma za Mama na Mtoto** | | | WORLD BANK | | 25,000,000 | 25,000,000 |
| | **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | 35,000,000 | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | 6,475,000 | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | **Programu ya Jamii ni Afya** | 1,500,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar** | 500,000 | 1,000,000 | PHARM ACCESS INTERNATIONAL | 528,800 | | 1,528,800 |
| | **Programu ya Kuimarisha Nguvu Kazi** | | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | i) Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | ii) Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | | 14,400,000 | BADEA/SAUDI FUNDS/ KUWAIT FUNDS | | 10,000,000 | 24,400,000 |
| | iii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia - Bunguni | | 1,700,000 | ECDF KOREA (EXIM BANK) | | 15,864,093 | 17,564,093 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **73,000,000** | **83,450,000** | | **53,927,202** | **50,864,093** | **188,241,295** |
| **H02** | **HOSPITALI YA MNAZI MMOJA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ununuzi wa Vifaa Tiba | 2,000,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,000,000** | **2,000,000** | | - | - | **2,000,000** |
| **N02** | **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi** | 40,000,000 | 300,120,000 | | | | 300,120,000 |
| | **Programu ya Upangaji wa Miji na Usimamizi wa Ardhi** | | 35,565,000 | | | | 35,565,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Taarifa za Ardhi Zanzibar (LARIS) | 5,000,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **45,000,000** | **335,685,000** | | - | - | **335,685,000** |
| **R01** | **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanda** | | | | | | |
| | i) Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks) | 40,320,000 | 35,560,000 | | | | 35,560,000 |
| | **Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar** | 10,000,000 | 10,803,870 | | | | 10,803,870 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **50,320,000** | **46,363,870** | | - | - | **46,363,870** |
| **K01** | **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu** | 234,389,998 | 247,647,900 | AfDB/WB/ BADEA/SIDA-GPE/ UNICEF | 31,969,564 | 159,706,123 | 439,323,587 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzi na Kufundishia | 49,405,000 | 39,208,100 | SIDA/GPE/ UNICEF/KFHI/ AUSTRIA/ UNICREDIT BANK | 280,500 | 8,661,453 | 48,150,053 |
| | ii) Uimarishaji wa Elimu ya Juu | 25,000,000 | 35,000,000 | | | | 35,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **308,794,998** | **321,856,000** | | **32,250,064** | **168,367,576** | **522,473,640** |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| J03 | **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | 60,000,000 | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | | 40,550,000 | GERMANY/GIZ | 633,982 | | 41,183,982 |
| | ii) Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Michezo | | 372,900,000 | | | | 372,900,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni | 5,000,000 | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | ii) Ujenzi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili | 4,500,000 | 16,500,000 | | | | 16,500,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **69,500,000** | **432,950,000** | | **633,982** | **-** | **433,583,982** |
| L01 | **WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji** | | | KOREA | | 5,806,218 | 5,806,218 |
| | **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo** | | | | | | |
| | i) Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu | 2,500,000 | 2,500,000 | | | | 2,500,000 |
| | ii) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki | | | ENABEL | 100,000 | | 100,000 |
| | iii) Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP) | | | IFAD/OPEC | | 5,250,000 | 5,250,000 |
| | iv) Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji | | 200,000 | KOREAN GOVERNMENT (KRC) | 3,750,000 | | 3,950,000 |
| | **Programu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Chakula** | | | | | | |
| | i) Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula | 27,500,000 | 20,000,000 | | | | 20,000,000 |
| | ii) Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP) | | | WB | | 12,500,000 | 12,500,000 |
| | iii) Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi (FOLUR) | | | GEF/WWF | 1,200,000 | | 1,200,000 |
| | iv) Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi | | | FAO/ILO/UNIDO /UNCDF/UN-WOMEN | 1,441,750 | | 1,441,750 |
| | v) Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha Usalama wa Chakula (STREPHIT) | | | EU | 2,365,590 | | 2,365,590 |
| | **Miradi** | | | | | | |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | i) Kuanzisha Bustani ya Mimea (Botanic Garden) | | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | ii) Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo (ENSURE) | | | ADF, EAC | 400,000 | | 400,000 |
| | iii) Kuimarisha Usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufu - Pongwe | | | WCS | 120,000 | | 120,000 |
| | iv) Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakabali wa Sekta ya Kilimo | | | | 549,045 | | 549,045 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **30,000,000** | **24,700,000** | | **9,926,385** | **23,556,218** | **58,182,603** |
| **H04** | **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Hifadhi ya Wazee | 4,500,000 | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | ii) Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana | | | EU/ UN WOMEN | 636,321 | | 636,321 |
| | iii) Mradi wa Kusimamia Sheria ya Jinsia na Sera | | | UNICEF | | | - |
| | iv) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | | | WORLD BANK | 529,200 | 3,825,000 | 4,354,200 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **1,500,000** | | **1,165,521** | **3,825,000** | **6,490,521** |
| **N03** | **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | |
| | **Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 10,154,964 | | | | | - |
| | ii) Uhuishaji na Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar | 2,850,000 | 2,516,670 | INDIA (EXIM BANK) | | 13,650,000 | 16,166,670 |
| | iii) Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi katika Maeneo ya Mijini | | | GIZ/KFW | 2,008,790 | | 2,008,790 |
| | iv) Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDFIP) | | 1,541,000 | JICA | | 39,949,745 | 41,490,745 |
| | vi) Ununuzi wa Chlorine, Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji | | | UNICEF | 40,000 | | 40,000 |
| | vii) Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar | 30,500,000 | 15,776,890 | | | | 15,776,890 |
| | viii) Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja | | 2,600,000 | | | | 2,600,000 |
| | ix) Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar | | 2,600,000 | KFW | 68,828,885 | | 71,428,885 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | x) Kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar | | | GERMANY/KfW | 3,362,953 | | 3,362,953 |
| | xi) Usimamizi wa Rasilimali Maji Chini ya Ardhi | | | | 1,682,856 | | 1,682,856 |
| | **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 33,000,000 | 7,000,000 | | | | 7,000,000 |
| | ii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) | 4,000,000 | | BENKI YA DUNIA | | 6,474,289 | 6,474,289 |
| | iii) Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar | | 33,355,685 | | | | 33,355,685 |
| | iv) Ulazaji wa Waya wa Umeme Baharini | | | AfDB/JICA/EU | | 3,969,000 | 3,969,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **80,504,964** | **65,390,245** | **-** | **75,923,484** | **64,043,034** | **205,356,764** |
| **L02** | **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi** | | | IFAD | | 13,138,491 | 13,138,491 |
| | **Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) | 4,000,000 | 7,000,000 | | | | 7,000,000 |
| | ii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji | 4,000,000 | | | | | - |
| | iii) Usambazaji wa Gesi | | 9,000,000 | | | | 9,000,000 |
| | **Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Mazao ya Baharini** | | | | | | |
| | i) Uanzishwaji wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara Uthamini wa Ubora wa Mazao ya Baharini | 4,000,000 | | | | | - |
| | ii) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mwani (SESEP) | | 6,575,000 | | | | 6,575,000 |
| | iii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | | | KOICA | 2,685,000 | | 2,685,000 |
| | iv) Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania - TASFAM | | | WB (IDA) | | 10,000,000 | 10,000,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Uvuvi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba | | 29,994,810 | | | | 29,994,810 |
| | ii) Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | 27,000,000 | 27,675,560 | | | | 27,675,560 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | iii) Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki | | 51,000,000 | | | | 51,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Utafiti wa Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii - SAMAKI | | | NORAD | 13,000 | | 13,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **39,000,000** | **131,245,370** | | **2,698,000** | **23,138,491** | **157,081,861** |
| **P01** | **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Barabara Kuu | 115,540,131 | 133,392,956 | BADEA/SF/ UKEF/ DEUTCH BANK /EXIM BANK OF CHINA | | 195,638,911 | 329,031,867 |
| | ii) Ujenzi wa Barabara za Ndani | 45,600,000 | 78,034,000 | | | | 78,034,000 |
| | iii) Matengenezo ya Barabara za Mjini | 112,092,000 | 35,000,000 | | | | 35,000,000 |
| | iv) Ujenzi wa Misingi ya Maji, Barabara pamoja na Matengenezo ya Maziwa katika Maeneo ya Mji | | 270,000,000 | | | | 270,000,000 |
| | **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | | BENKI YA DUNIA | | 140,000,000 | 140,000,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 9,500,000 | 2,000,000 | UKEF/CITI BANK | | 159,500,000 | 161,500,000 |
| | ii) Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA | 26,000,000 | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |
| | iii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA (Phase II) | | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |
| | iv) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi | | 22,500,000 | | | | 22,500,000 |
| | v) Ujenzi wa Apron katika kiwanja cha Ndege cha AAKIA | | 40,000,000 | | | | 40,000,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha Bandari** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 157,539,960 | 205,100,364 | | | | 205,100,364 |
| | ii) Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi | | | NETHERLAND | 130,000,000 | | 130,000,000 |
| | **Programu ya Mageuzi ya Kidigitali** | | | | | | |
| | i) Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini Zanzibar (International Gateway) | | 30,000,900 | | | | 30,000,900 |
| | ii) Utoaji wa Huduma ya Mtandao katika Maeneo ya Umma (Public Wi-Fi ) | | 10,050,000 | | | | 10,050,000 |
| | iii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Data | | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |

| KIFUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA | MAKISIO YA SMZ KWA | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | iv) Uimarishaji Mfumo wa Mawasiliano | 6,000,000 | 6,000,000 | | | | 6,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Uwekaji wa Kamera za Kusimamia Usafiri Barabarani | | 1,873,000 | | | | 1,873,000 |
| | ii) Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma | | | SPAIN | 374,338 | | 374,338 |
| | iii) Ununuzi wa Boti Mbili za Serikali | 26,000,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **498,272,091** | **923,951,220** | | **130,374,338** | **495,138,911** | **1,549,464,469** |
| **J01** | **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria** | 15,000,000 | 6,000,000 | | | | 6,000,000 |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii** | | 6,000,000 | | | | 6,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe | 9,000,000 | 10,000,000 | | | | 10,000,000 |
| | ii) Ukarabati wa Jengo la Beit Al Ajaib | | | SULTANATE OF OMAN | 15,025,822 | | 15,025,822 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **24,000,000** | **22,000,000** | | **15,025,822** | - | **37,025,822** |
| | **JUMLA YA KUBWA** | **1,862,000,000** | **3,231,400,000** | - | **345,498,127** | **962,742,151** | **4,539,640,278** |
| | **JUMLA YA FEDHA ZA WAHISANI** | | | | | **1,308,240,278** | |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | | | | **4,539,640,278** |